# MTUME MUHAMMAD

## S.A.W.

# KATIKA BIBLIA

Kimetungwa na:
Sheikh Muhammad Ishaque Soofi, B. A.

**Kimeenezwa na:**
**Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya**
**S.L.P. 376, Dar es Salaam**
**TANZANIA**

## TAFADHALI SOMA HAYA KWANZA

Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya inafanya kazi ya kuuinua Uislamu katika Afrika Mashariki tangu miaka 34. Maelfu ya vitabu na magazeti yanayopigwa chapa kila mwaka yanashuhudia wazi wazi kwamba Jumuiya hii peke yake imejitolea kwa kuitumikia dini ya Kiislamu katika Afrika ya Mashariki.
Hakuna Jumuiya nyingine ya Kiislamu iliyoanza kazi mapema tangu 1934 wala hakuna Jumuiya nyingine iliyo na mpango wa kuulinda Uislamu na mashambulio ya maadui zake.

Nabii Isa a.s. alisema, “Mti hujulikana kwa matunda yake”. Hivyo, msomaji mpenzi, usiendelee kudanganywa na wapinzani wa Jumuiya hii ambao wamekula fedha nyingi za Waislamu wa nchi hii na wa nchi zingine bila kuleta matokeo mema. Tafadhali zinduka. Usikubali kupumbazwa na watu werevu wasioelewa dini vizuri wala hawana moyo wa kuusaidia Uislamu. Fanya haraka kujiunga na Jumuiya ya Ahmadiyya nawe utaona kuwa unatembea katika mwangaza na Ushindi wa Uislamu utapatikana kwa kujiunga na Jumuiya ya Ahmadiyya tu.

Wako,

Sheikh Muhammad Ishaque Soofi (B.A.).
Amir na Mbashiri Mkuu.
Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya.
Uganda

Uganda Ahmadiyya Muslim Mission
27, GOKHLE ROAD EAST,
Sanduku la Posta: 95, JINJA,
UGANDA.

## YALIYOMO

Neno la mbele ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... iii

**SEHEMU YA KWANZA**

1. Kusudi la kitabu hiki ... ... ... ... ... ... ... 1
2. Muhammad s.a.w. katika Biblia ... ... ... ... 3
3. Bishara ya kwanza ... ... ... ... ... ... ... 4
4. Bishara ya pili ... ... ... ... ... ... ... ... ... 7
5. Bishara ya tatu ... ... ... ... ... ... ... ... 9
6. Bishara ya nne ... ... ... ... ... ... ... ... ... 9
7. Bishara ya tano ... ... ... ... ... ... ... ... 10
8. Bishara ya sita ... ... ... ... ... ... ... ... ... 13
9. Bishara ya saba ... ... ... ... ... ... ... ... 19
10. Bishara ya nane ... ... ... ... ... ... ... ... 21
11. Bishara ya tisa ... ... ... ... ... ... ... ... 22
12. Bishara ya kumi ... ... ... ... ... ... ... 22
13. Bishara ya kumi na moja ... ... ... ... ... ... 24
14. Bishara ya kumi na mbili ... ... ... ... ... ... 25
15. Bishara ya kumi na tatu ... ... ... ... ... ... 27

16 Kuja kwa Nabii Muhammad s.a.w ... ... ... 31

**SEHEMU YA PILI**

1. Hadhrat Ahmad a.s. - Masihi wa Nabii Muhammad s.a.w. ... ... ... ... ... ... ... ... ... 35
2. Bishara za kuja kwa Mahdi aliyeahidiwa .. ... 40

## NENO LA MBELE

Kitabu hiki ambacho nina heshima kukiweka mbele ya wasomaji wangu wapenzi kiliandikwa nami wakati nilipokuwa Mbashiri Mkuu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya katika nchi ya Kenya miaka 1964 - 1967. Baada ya kuandika madhumuni ya kitabu hiki katika lugha ya Kiingereza, nilimwomba ndugu yangu mpenzi Bwana Athumani Gakuria wa idara ya elimu, Nairobi, kufasiri ibara yake katika lugha ya Kiswahili.
Yeye alinifanyia hisani kukubali ombi langu kwa furaha na kufasiri kitabu hiki katika lugha ya Kiswahili. Yeye hakufasiri tu kitabu hiki bali aliongeza maneno mengi yenye manufaa juu ya madhumuni yangu na kwa hiyo mimi ninamshukuru sana sana, namwomba Mwenyezi Mungu abariki katika umri wake na kazi yake ambayo yeye amefanya kwa ajili ya kueneza dini ya Kiislamu. Amin.

Mimi ninamshukuru Alhaj Ibrahim Senfuma wa Buvunya, Uganda ambaye, pamoja nami, alisoma, ukurasa kwa ukurasa, madhumuni ya kitabu hiki. Na kadhalika ninawashukuru Shaikh Jamil-ur-Rahman Rafiq, B.Sc., Mbashiri Mkuu katika nchi ya Tanzania, Shaikh Muhammad Munawwar Mbashiri Maarufu wa Afrika ya Mashariki, Bwana Hemedi Mbyana na Sharif Husain Saleh Hafidh wa Mombasa ambao walifanya juhudi kubwa kwa kusahihisha kitabu hiki kabla ya kuchapishwa. Mwenyezi Mungu Awabariki hawa wote. Amin.

Madhumuni ya kitabu hiki ni muhimu sana na kwa hiyo mimi sina shaka hata kidogo ya kwamba Waislamu wote katika Afrika ya Mashariki watafahamu uzuri wa madhumuni hii na kupata manufaa makubwa kwa kuisoma. Wao watajua ya kwamba baada ya kusoma kitabu hiki watapata nguvu zaidi ya kujadiliana na Wakristo na kuwaingiza upesi katika dini ya Kiislamu.

Ikumbukwe hapa ya kwamba msingi wa madhumuni ya kitabu hiki ni juu ya vitabu hivi vitatu.

1. "Introduction to the Study of the Holy Quran" Kilichotungwa na Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad. Khalifat-ul-Masih II, Mungu awe radhi naye.

2. "Bible Ki Basharat" (KIURDU) kilichoandikwa na Marehemu Hadhrat Dr. Mufti Muhammad Sadiq. Mbasbiri wa kwanza wa Kiahmadiyya aliyepelekwa Amerika.

3. Tafsiri ya Kurani Tukufu kwa Kiswahili ya Shaikh Mubarak Ahmad. Mbashiri wa kwanza kuletwa Afrika Mashariki.

Mwishoni namwomba Mwenyezi Mungu Ajaalie kitabu hiki kiwe chenye manufaa makubwa kwa ajili ya kueneza dini ya Kiislamu katika Afrika ya Mashariki na kwingineko. Amin.

Mtumishi wa Uislamu.
Muhammad Ishaque Soofi, B.A.,
Amir na Mbashiri Mkuu,
Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya,
Uganda.

Ahmadiyya Muslim Mission,
27, Gokhle Road, East,
Jinja, Uganda.
1969 A.D.

بِسْمِ اللهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ

Kwa jina Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema Mwingi wa ukarimu.

## SEHEMU YA KWANZA

## KUSUDI LA KITABU HIKI

Lengo la kitabu hiki ni kuthibitisha zile bishara za Biblia zilizotimia kwa kufika Nabii Muhammad (s.a.w.), Mtume Mtukufu wa Uislam. Kadhalika tutatoa maoni ya Kiislam juu ya Biblia ili mtu asije kutulaumu sisi Waislamu kwa kuthibitisha ukweli wa Nabii Muhammad s.a.w. tukitumia bishara za Kitabu tusichoamini kuwa ni UFUNUO wa Mungu sawa sawa. Jambo hili laweza kuleta wasiwasi katika nyoyo za watafutao haki, hivyo maoni ya Waislamu ni ya muhimu sana katika mradi wa kitabu hiki na lastahili kuelezwa kwa uwazi iwezekanavyo.

Miongoni mwa nguzo sita za imani ya Kiislam, kuna nguzo hizi mbili, "Kuamini Manabii wa Mwenyezi Mungu na kuamini Vitabu vya Mwenyezi Mungu." Manabii kama Musa, Daudi, Suleimani na Yesu, na wengine waliotajwa katika Biblia wote wanaaminiwa na kuheshimiwa na kila Mwislamu safi. Waislamu wote wanaamini ya kuwa Manabii hao wote walipata ufunuo toka kwa Mwenyezi Mungu. Mara tu itakapothibitishwa ya kwamba ule ufunuo walipata wao wenyewe au kusimamia kuandikwa kwake Vitabu walipokuwa hai. Waislamu hawatasita kuukubali. Lakini kwa bahati mbaya, maneno ya Biblia si yote yaliyofunuliwa na Mwenyezi Mungu kwa mitume wake. Historia ya Biblia inaonyesha ya kuwa hii Biblia tulilyo nayo iliandikwa kufuatia masimulizi ya nyakati mbalimbali za karne nyingi, na imefanyiwa mabadiliko makubwa, mipachiko na machafuo.

Wataalamu wa Historia ya Biblia wanatuambia Agano la Kale la Kiebrania limo katika maandiko yaliyoandikwa yapata karne 5 au 8 baada ya kufariki Yesu - walakini hata kabla ya hapo, kwa

sababu kadha wa kadha, ni wazi kwamba michafuo mingi ilifanywa ndani ya maandiko hayo ya Kiebrania (Encyclopaedia Britanica, Chapa ya II - chini ya neno Bible).

Hii ndiyo hali ya Agano la Kale. Hebu sasa tulichunguze Agano Jipya lililoandikwa baadaye na ndiyo maandiko matakatifu ya Wakristo.

Mtaalamu mashuhuri wa huko Oxford ameandika haya katika kitabu chake "The Story Behind the Gospel" yaani (Hadithi ya Undani wa Injili). "Jambo la maana ni kukumbuka ya kuwa hakuna hata Injili moja iliyopata kuandikwa mpaka miaka mingi sana baada ya kifo cha Yesu. Kwa ujumla Injili ya Marko ndiyo inayodhaniwa kuwa ya zamani zaidi. Inakadirwa kuwa iliandikwa mnano 65 A.D. baada ya kuzaliwa Yesu. Tarehe ya kusulubiwa kwa Yesu inafikiriwa kuwa labda 29 au 30 A.D. Hivyo Injili hii iko kama miaka 35 hivi nyuma ya habari inazozieleza. Injili zilizobaki ziliandikwa miaka mingi baadaye.

"Katika miaka ya mwanzo iliyofuatia kifo cha Yesu hapakuwepo na maandiko yoyote juu ya maisha na mafundisho ya Yesu. Pengine baadhi ya methali zake mashuhuri zilikuwa zimeingizwa katika ibara fulani fulani.

Lakini kadri miaka ilivyozidi kupita na maneno ya Yesu kuzidi kusahaulika ilionelewa heri kuyaandika. Usahihi wa maandiko hayo awali ulikuwa ni lazima utegemee maoni ya wale walioweza kukumbuka maneno ya Yesu, kama ilivyokuwa zama zile, na pia masimulizi ya wale waliokua na Yesu na kumsikia, na Injili za leo zimeandikwa kufuatia visa na masimulizi haya.

"Tunapokumbuka ya kuwa habari, hata ikiwa ni juu ya jambo lililotendeka hivi punde tu, ni vigumu sana kupita kinywa hata kinywa bila ya kupata mabadiliko. Hivyo linakuwa ni jambo lisilopingika ya kwamba masimulizi ya Yesu yalivyopitia kinywa hiki hadi kile kwa muda wa miaka thelathini (katika zama za giza) yalipata mabadiliko makubwa katika muda huo wote. Kadhalika yatupasa tukumbuke ile desturi ya waandishi wa kale, kwani wao walipoandika habari za mtu fulani walitumia maneno waliyoona

yanatimiza mradi wao bila ya kukusudia kudokeza ya kuwa hayo ni sahihi na ni yale yale aliyoyatamka yule mtu mwenyewe. Wala hapakuwa na mwandishi wa kale aliyekuwa mwangalifu hivi kwamba aliyachungua na kuyakariri maandiko yake hata yakaweza kufafanua mradi kamili wa jambo alilokusudia kueleza. Bila shaka Injili, ambazo hazikuandikwa kama kumbukumbu tu bali kama mafundisho pia, zilihusikana sana na tabia hii ya mwandishi wa kale.

"Kwa hivyo hatuna usalama wowote ya kuwa visa na methali kama tusomavyo katika Biblia zinawakilisha matendo hasa yaliyotendeka na maneno ya asili yaliyonenwa," (The Story Behind the Bible, by Mr. Allen, ukurasa 44).

Kufuatia mazungumzo ya hapo, ni wazi ya kuwa Biblia, kama tuijuavyo si maneno ya ufunuo wa Mwenyezi Mungu. Biblia ni hati iliyoandikwa na watu kufuatia mila na methali iliyorithiwa toka kizazi hata kizazi. Karne nyingi zilipita kabla Biblia haijaingia katika sura yake ya hivi sasa, na katika muda huo mrefu, ilifanyiwa mabadiliko mengi, mipachiko na machafuo chungu nzima. Katika hali hii Biblia kimekuwa kitabu kinachokusanya ukweli uliochanganyika na uzushi, upungufu na maneno yasiyopatana. Baadhi ya ukweli uliomo Bibliani, ni bishara ambazo katika hizo nyingi zilitimia kwa kufika kwake Mtume Muhammad s.a.w. Katika kitabu hiki tutadhihirisha kwa uwazi kutimia kwa fungu kubwa la bishara hizo. Nasi hatuna budi kuingilia jambo lenyewe sasa.

## MUHAMMAD S.A.W. KATIKA BIBLIA

Kuja kwa Nabii Muhammad s.a.w. si jambo geni kwa watu wa Kitabu maana kumebashiriwa mara nyingi katika Biblia. Haya yanathibitishwa na Qur'an Tukufu inayosema hivi juu ya waaminio kwamba ni wale "Ambao wanamfuata Mtume, Nabii aliye Ummi, ambaye wao humkuta ameandikwa kwao katika Taurati na Injili. Huwaamuru yaliyo mema na kuwakataza yaliyo mabaya." (7:158).

Maneno haya "Ameandikwa kwao katika Taurati na Injili", yanaonyesha kwamba Nabii Muhammad s.a.w. si Mtume wa kitaifa bali ametumwa kwa mataifa yote ya wanadamu.

Mtume Muhammad s.a.w. kwa kuwa ni m'bora wa mitume wote (Sura 33:41) naye alitumwa kwa watu wote (Sura 7:159) bishara zinazotabiri kuja kwake zinapatikana katika vitabu vya dini zote. Hapa vimetajwa Taurati na Injili. Katika vitabu hivyo mna bishara nyingi zenye kuwawezesha Mayahudi na Wakristo kumtambua Mtume Muhammad s.a.w. Hapa tutaeleza baadhi ya bishara hizo.

## BISHARA YA KWANZA.

Siku ya mkutano katika Horeb, wana wa Israeli walipokataa kusikia sauti ya Mwenyezi Mungu. Mungu alimwambia Musa. "Wametenda vema kusema walivyosema, mimi nitawaondokeshea nabii miongoni mwa ndugu zao mfano wako wewe, nami nitatia maneno yangu kinywani mwake. naye atawaambia yote nitakayomwamuru. "Hata itakuwa, mtu asiyeyasikiliza maneno yangu atakayoyasema yule kwa jina langu, nitalitaka kwake. Lakini nabii atakayenena neno kwa kujikinai kwa jina langu, ambalo sikumwagiza kulinena, au atakayenena kwa jina la miungu wengine, nabii yule atakufa." (Kumbukumbu la Torati 18.16-20).

Bishara hii tukufu inaonyesha mambo haya yafuatayo.

(i) Wana wa Israeli hawatasikia tena sauti yenye nguvu ya Mwenyezi Mungu.
(ii) Anayebashiriwa kufika ni Nabii.
(ill) Ataondokeshwa miongoni mwa ndugu wa Waisraeli.
(iv) Atakuwa mfano wa Musa.
(v) Maneno atakayoyasema yatakuwa ufunuo wa Mungu.
(vi) Atawaambia yote atakayoambiwa na Mungu.
(vii) Atanena hayo kwa jina la Mungu.
(viii) Asiyetaka kusikia maneno hayo ataadhibiwa.
(ix) Nabii wa uwongo atakayesingizia kutumwa na Mungu atakufa.
(x) Atakayesema kwa jina la miungu wengine atauawa.

Sasa ni watu wawili wanaosemwa kuwa wametabiriwa katika bishara hiyo. Wakristo wanasema ni Yesu, na Waislamu tunasema ni Muhammad s.a.w. Bishara yenyewe haitaji jina la mtu ye yote, ila tu imeeleza alama kumi za Nabii huyo.
Basi tupeleleze alama hizo zinamwangukia nani katika manabii hawa wawili.

(i) Katika bishara hiyo Waisraeli wanaambiwa kwamba hawatasikia tena sauti ya Mungu. Na inajulikana pote ya kuwa Yesu alikuwa Mwisraeli aliyezaliwa katika ukoo wa Daudi (Mathayo. 1:1). Mtume Muhammad s.a.w. alikuwa Mwarabu. Hakuwa katika kizazi cha Waisraeli kilichonyimwa baraka za Mungu, kwa kukataa kwao kusikia sauti ya Mungu.

(ii) Bishara inasema huyo anayebashiriwa kufika ni nabii. Wakristo wanaamini ya kwamba Yesu alikuwa "Mungu-Mwana" au Mungu Mwenyewe, nao hawataki kabisa Yesu aitwe nabii. Lakini Mtume s.a.w. aliitwa *Rasuulullaahi* (Mtume wa Mungu) na pia *Nabiyyullaahi* (Nabii wa Mungu).

(iii) Ikumbukwe kwamba nabii Ibrahim - baba wa manabii - ndiye aliyemzaa Ismaeli na Isihaka. Wazao wa Ismaeli ndio Waarabu, na wazao wa Isihaka ndio Waisraeli. Mtume Muhammad s.a.w. alitokana na Waismaeli ambao ni ndugu wa Waisraeli, kama inavyoagua bishara hiyo. Lakini Yesu mwenyewe ni Mwisraeli, wala hakutoka katika ndugu wa Waisraeli. Hivyo bishara hii si yake.

(iv) Bishara inaeleza tena ya kuwa mtume huyo atakuwa mfano wa Musa. Nasi tunaona ya kuwa Mtume Muhammad s.a.w. ndiye anayeitwa mfano wa Musa katika Kurani tukufu (sura 73:16). Yesu angewezaje kujifanya kama Musa hali mwenyewe alikuwa chini ya Sheria ya Musa? (Mathayo 5:17, 7:12, Marko 10:19. Matendo 24:14). Hali ya Mtume Muhammad s.a.w. na ya Nabii Musa zinafanana sana. Nabii Musa alizaliwa na wazazi wawili wala hakulaumiwa katika kuzaliwa kwake. Tena Musa alioa, alipewa

Sheria mpya, alihama nchi yake baada ya kupewa utume, alipigana na adui zake, nao wakaangamia mbele ya macho yake, alikufa kifo cha kawaida, walitokea maimamu na mawalii katika umati wake, na mwishowe alikuja Masihi kusimamisha Sheria ya Musa. Hayo yote yalipatikana kwa Mtume Muhammad s.a.w. na hivyo wamefanana kabisa. Lakini hakuna hata alama moja ya hizo inayopatikana katika dhati ya Yesu sawa na itikadi za Wakristo.

(v) Bishara inaendelea kusema: “Nami nitatia maneno yangu kinywani mwake”. Yaani Mungu atamteremshia maneno yake. Alama hii pia haionekani katika Yesu. Wakristo wanaamini ya kuwa Yesu alikuwa Mungu, kwa hivyo hakukuwa na haja ya kufunuliwa maneno kutoka kwa Mungu. Zaidi ya hayo, Kurani ndiyo Sheria ya pekee inayostahili kuitwa “Maneno ya Mungu”, maana haina hata neno moja lisilotoka kwa Mungu Mwenyezi.

(vi) Mtume s.a.w. anaambiwa na Mwenyezi Mungu kufikisha yote aliyoteremshiwa (Kurani tukufu 5.68). Yesu aliwaambia wanafunzi wake ya kuwa hatawaambia yote (Yohana 16.12-13). Hivyo bishara hii haimhusu Yesu.

(vii) Alama ya saba pia haionekani katika Yesu. Mtu anayesoma Injili anajua ya kwamba Injili yo yote haikuanzishwa kwa jina la Mungu. Yesu anasema mara kwa mara. “Bali mimi nawaambieni” (Mathayo 5:22. 28, 34. 39. 44). Luka anasema, ameandika Injili yake kwa sababu. “Nimeona vema mimi nami kwa kuwa nimejitafutia usahihi wa mambo hayo yote tangu mwanzo, kukuandikia kwa taratibu, Theofile Mtukufu” (Luka 1:3-4). Hasemi kwamba alifunuliwa na Mungu, au ameongozwa na Roho Mtakatifu, wala hakuandika Injili hiyo ili watu wote waisome, bali alimwandikia mtu mmoja tu, Theofile. Paulo alisema. “Kwa habari za wanawali, sina amri ya Bwana. Lakini natoa shauri langu” (Wakorintho 7:25). Ni dhahiri ya kwamba Injili za leo ni mkusanyiko wa maneno ya watu mbali mbali. Lakini Kurani inataja jina la Mwenyezi Mungu katika mwanzo wa kila sura, na inaonekana Mungu alikusudia

kutimiza alama hiyo wazi wazi. Tena Mtume s.a.w. kabla ya kuanza kazi yo yote alikuwa anataja jina la Mwenyezi Mungu.

(viii) Waliokataa kusikiliza maneno ya Mungu yaliyotoka kinywani mwa Mtume s.a.w. waliadhibiwa hapa hapa duniani. Vita vikali vilivyoangamiza maadui wa Uislamu vilikuwa adhabu ya Mwenyezi Mungu iliyoahidiwa katika bishara hii, na bado kuna adhabu ya akhera itakayowawakia walio maadui wa haki.

(ix) Wapinzani wa Uislamu wanasema ya kwamba Mtume s.a.w. alizua uwongo. Bishara hii inawajibu na kusema mtu ye yote atakayemzulia Mungu atauawa. Mtume s.a.w. alikaa miaka mingi duniani na akisha maliza kazi yake akafariki kifo cha kawaida. Lakini Yesu je? Tukifuata imani ya Wakristo kuwa aliuawa msalabani, tunashurutishwa kusema ya kuwa (Mungu apishe mbali) alikuwa mwongo, maana bishara yasema kuwa nabii wa uwongo ndiye atauawa. Hivyo kufaulu kwa Mtume s.a.w. na maendeleo ya kazi yake ni dalili zilizo wazi za ukweli wake.

(x) Bishara inaeleza tena ya kuwa mwenye kusema neno kwa jina la miungu wengine "Nabii yule atakufa". Kwa kuwa Mtume s.a.w. hakuuawa basi imethibitika ya kwamba yote aliyosema alifunuliwa na Mungu.

## BISHARA YA PILI.

Katika kumbukumbu la Taurati 33:2-3 imeandikwa hivi, "Bwana alitoka Sinai, akawaondokea kutoka Seiri, akaangaza kutoka kilima cha Parani, na akaja na elfu kumi za watakatifu. Upande wa mkono wake wa kuume palikuwa na sheria ya moto moto kwao. Hakika awapenda hayo makabila ya watu, watakatifu wake wote wamo mkononi mwako, nao waliketi miguuni pako".

Hapa pameelezwa maonyesho matatu ya Mwenyezi Mungu. Musa alitoka Sinai. Seiri ni alama ya Yesu. Na Mtume Muhammad s.a.w. aliangaza kutoka kilima cha Parani. Wanazuoni wamekubali

ya kwamba Parani ni kilima cha Makka (Mu'jamul Buldaan). Biblia inasema. Ismaili "akakaa katika jangwa la Parani" (Mwanzo 21:21) na Mtume Muhammad s.a.w. ni mjukuu wa Ismaili.

Mtume s.a.w. alipoondoka Madina kwenda kuiteka Makka alikuwa na masahaba elfu kumi. Katika Biblia ya Kiingereza hesabu ya watakatifu hao imetajwa kuwa *"ten thousand saints"* yaani "watakatifu elfu kumi", kama tulivyofasiri hapo juu. Lakini katika Biblia ya Kiswahili cha Mvita (Mombasa). Wamefasiri maneno hayo kuwa "Makumi ya elfu", yaani elfu zile zilikuwa si kumi moja bali makumi mengi, wapate kuwavuruga wasomao Kiswahili wasijue hesabu ya Masahaba watakatifu wa Mtume s.a.w. aliotokea nao Parani katika bishara ya Biblia. Inasikitisha kuona ya kwamba Mapadri hawajatosheka na kiasi hicho cha mageuzi. Katika tafsiri mpya ya Biblia (Union Version) ya mwaka 1952 kifungu hicho cha maneno wamekiandika: "Akaja Meribath kadeshi", ili wavuruge kabisa bishara hiyo isiweze kufafanuka. Ni ajabu maneno kama *Tirshatha* (uk. 478), *Darkoni* (uk. 479) na mengine yameelezwa chini katika kurasa, na mengine yameelezwa mwisho wa kitabu cha Biblia, lakini neno Meribath-kadeshi hawakulieleza chini ya ukurasa ule wala mwisho wa kitabu. Ingawa ni jipya kabisa lakini limefanywa lionekane kama jina la mtu au Malaika au hivi. Wale wanaofikiri ya kwamba Biblia ya Union Version imefasiriwa vizuri sana katika Kiswahili cha kisasa, watasemaje juu ya uaminifu huu wa wafasiri? Ilikuwaje wanazuoni wakubwa wakubwa wa Kiyunani na Kiebrania na Kiswahili kushindwa kufasiri au kueleza neno Meribath-kadeshi? Inaonekana dhahiri ya kwamba dhamiri za mapadri zinawalaumu juu ya tafsiri zao zisizo sahihi, zinazovurugwa ili kuficha haki.

Alama nyingine ni kuleta Sheria. Mtume Muhammad s.a.w. ndiye aliyeleta Sheria baada ya Nabii Musa. Na ile Sheria ilileta joto katika mioyo ya Waislamu, nao wakainuka katika miaka michache. Pia imeitwa "Sheria ya Moto Moto" kwa ajili ya kuunguza maovu, madhambi na mabaya yote. Wale waliojaribu kuipinga

Kurani wakaangamia wenyewe. Kweli, Kurani ikifuatwa sawa sawa, inaweza kuchoma dhambi za watu kama moto unavyochoma takataka. Je hamwoni Waarabu waliokuwa wakinywa ulevi kutwa mara tano waliacha wakawa wanasali kutwa mara tano?

Mtume alizipenda sana kabila zote. Katika masahaba wake kulikuwa Waarabu wa makabila mbali mbali: Wahabeshi, Waajemi na Warumi, na Mtume s.a.w. aliwapenda wote. Hakuwaita mbwa na nguruwe watu wa mataifa mengine kama alivyowaita Yesu (Mathayo 7:6; 15:26).

Masahaba wa Mtume s.a.w. pia walimpenda sana. Kwa hakika Mtume s.a.w. alipendwa na masahaba zake zaidi kuliko kila mtu anavyopendwa na wafuasi wake. Katika vita, kama mishale ilipigwa kutoka katika kila upande, masahaba walimzunguka Mtume kama kuta ili asipate kujeruhiwa. Hatuwezi kuwalinganisha na wanafunzi wa Yesu waliomtoroka wote wakakimbia na kumwacha Yesu peke yake katika matata (Mathayo 26:56. Marko 14:50).

**BISHARA YA TATU.**

Katika Wimbo ulio Bora (5:10) mmeandikwa "Mpenzi wangu ni mweupe tena mwekundu - mwekundu. Ndiye mkuu katika elfu kumi" (Biblia ya Kimvita).

Huyu aliyetajwa hapa na Nabii Suleimani aliyekuwa mkuu katika watu elfu kumi si mwingine bali Mtume Muhammad. Maneno ya mbele ya haya yameeleza sifa zote za mwili wa Mtume s.a.w. kama ulivyokuwa.

**BISHARA YA NNE.**

Isaya 28:9-13 kinasema, "Atamfundisha nani maarifa? Atamfahamisha nani habari hii? Je! ni wale walioachishwa maziwa, walioondolewa matitini? Kwa maana ni amri juu ya amri, amri juu

ya amri, kanuni juu ya kanuni, kanuni juu ya kanuni, huku kidogo na huku kidogo. La, bali kwa midomo ya watu wageni, na kwa lugha nyingine atasema na watu hawa; ambao aliwaambia, Hii ndiyo raha yenu, mpeni raha yeye aliyechoka; huku ndiko kuburudika; lakini hawakutaka kusikia.

“Kwa sababu hiyo neno la Bwana kwao litakuwa hivi, amri juu ya amri, amri juu ya amri; kanuni juu ya kanuni, kanuni juu ya kanuni; huku kidogo na huku kidogo, ili waende na kuanguka nyuma, na kuvunjwa, na kunaswa, na kuchukuliwa”.

Walioachishwa maziwa ni wana wa Ismaili ambao waliakhirishwa kupata ujumbe wa Mungu. Kurani tukufu iliteremshwa pole pole, amri juu ya amri, kama ielezavyo bishara hiyo. Baadhi ya sura zilishuka Makka na nyingine Madina (Huku kidogo na huku kidogo).

Kurani tukufu iliteremshwa katika lugha ya Kiarabu ambayo ni “Midomo ya watu wageni na lugha nyingine” kwa wana wa Israeli. Mbele imeelezwa ya kwamba Mtume s.a.w. atakimbilia Madina kwenye raha, mapumziko na maburudiko, lakini watu wa Makka watazidi kukataa ujumbe wa Uislamu mpaka watashindwa, kuvunjwa na kunaswa, na kuchukuliwa.

**BISHARA YA TANO.**

Katika Isaya 21.13-17 mmeandikwa: “Hili ni neno zito lililo juu ya Arabia. Ninyi mtalala ndani ya msitu wa Arabuni, enyi Wadedani wenye kusafiri pamoja, Wenyeji wa nchi ya Tema walimletea maji yule aliyekuwa na kiu, walimlisha mkate wao yule aliyekimbia.

“Kwani walizikimbia hizo panga, huo upanga uliofutwa, na huo uta uliopindwa, na hayo mazito ya vita. Kwani yeye Jehova ameniambia neno hili, katika muda wa mwaka mmoja, kwa kuandama hesabu ya miaka ya mwenye kuajiriwa, huo utukufu

wote wa Kedari utabatilika, na hao watakaosalia katika hesabu ya hao wenye kutumia uta, hao Mashujaa wa hao wana wa Kedari, watakuwa ni wachache kwa maana Jehova, yeye Mwenyezi Mungu wa Israeli, amenena neno hili.”

1. Aya 13 inatabiri juu ya “Hijra” yaani kuhama kwa Mtume Muhammad s.a.w. kutoka Makka hadi Madina. Tukio hili ni mojawapo katika matukio matukufu sana katika historia ya dini ya Kiislamu, maana Kalenda ya Kiislamu huanzia tangu wakati huo. Mtume s.a.w. alipotoka Makka kwa amri ya Mwenyezi Mungu na kuhamia Madina ambako alistawi sana na baadaye akiwa na masahaba wake watakatifu elfu kumi alirudi kuingia Makka bila kizuizi.

2. Maneno ya Aya 14 yanaeleza hali ya Mtume s.a.w. aliposafiri kuhamia Madina. Ikumbukwe ya kwamba Tema ndilo jina la nchi ambamo miji ya Makka na Madina yapatikana.

3. Maelezo ya aya 15, ni juu ya ile hali ya nchi yenye mateso na usumbufu juu ya Mtume s.a.w. ambayo watu wa Makka walimtendea hata maisha yake yakawa katika hatari katika mji huo alimozaliwa. Katika kitabu cha Maisha ya Mtume Muhammad, kilichoandikwa na marehemu Al-Haj F. R. Hakeem uk. 22 imesimuliwa hivi :-

“Mwisho saa ilifika. Wakimkuta Mtume s.a.w. akielekea kuwa peke yake kabisa, Wakubwa wa Kikureshi walifanya mkutano katika Dar-un-Nadwa.. ambako mambo ya kiserikali yalifikiriwa na mashauri kukatwa. Walikutana huko na kushauriana jambo gani afanyiwe. Baadhi yao walifikiri afungwe kamba na atupwe katika chumba cha giza na aachwe bila chakula mpaka afe. Wengine walifikiri asafirishwe mbali sana. Lakini, mwishowe Abu Jahli aliwapa mawazo yake ya kwamba vijana wa ukoo mkuu wapewe panga kali, ambao watatumia kwa kumhujumu kwamba wote watamshambulia wakati mmoja ili pasiwe na kabila maalumu la Makureshi la kushtakiwa kwa kuua.

Bani Hashim (Kabila la Mtume, s.a.w.) lingeridhika, kwa hivyo kupewa pesa za damu badala ya kuwaadhibu.

"Mpango huu ulikubaliwa na watu wote. Baadaye watu walio na silaha walijipanga nje ya nyumba ya Mtume s.a.w. tayari kumuua akitoka nje. Lakini Mwenyezi Mungu alimwepusha na hila zao mbaya na akamwepusha na panga zao zilizokuwa kali."

Hii ndiyo iliyokuwa hali ya mji wa Makka Mtume alipouhama, na hizi hasa ndizo hali zilizotabiriwa na maneno hayo ya Isaya.

4. Aya 16 yatabiri juu ya vita vya Badr, ambavyo Mtume s.a.w. na wafuasi wake wachache walipigana na kundi kubwa la maadui wa Uislamu mwaka mmoja baada ya Mtume kuhamia Madina. Katika vita hivi vilivyopiganwa karibu na mji wa Madina, Waislamu wachache waliokuwa na silaha haba waliwashinda maadui zao waliokuwa wengi sana tena mahodari wa vita.

Hesabu ya Waislamu ilikuwa 313 hali maadui zao walikuwa elfu moja. Lakini kwa kudra ya Mwenyezi Mungu, mwenye uwezo wote, maadui wa Uislamu walishindwa vibaya sana na bishara iliyotajwa hapo juu ikatimia barabara. Pia ikumbukwe ya kwamba Kedar ni jina la mtoto mmoja wa Ismaili ambaye wazao wake waliishi katika sehemu ya Hijaz ulipo mji wa Makka.

Wataalamu wa historia wamethibitisha kuwa Makureshi wa Makka (ambao ndio wale waliopeleka jeshi Madina kwenda kuwasaga Waislamu, lakini badala yake wakasagwa wao) walitokana na hao wazao wa Kedar. Na kule kushindwa kwao baada ya mwaka mmoja baada ya Mtume s.a.w. kuhamia Madina kunakamilisha bishara hii ya Isaya bila upungufu wo wote.

5. Ile aya ya mwisho, yaani 17, inatabiri ushindi wa Mtume s.a.w. juu ya maadui zake katika hivyo vita vilivyotokea mwaka mmoja baada ya Mtume kuhamia Madina.

Kwa jumla bishara hii nzima haina uhusiano wo wote na Nabii mwingine ila tu Nabii Muhammad s.a.w. Wala hapana ushahidi wa historia unaoweza kutufanya tuseme ya kwamba pana Mtume mwingine aliyehama mji wake kwa ajili ya maadui zake na kisha akawashinda hao hao baada ya mwaka mmoja. Hayo yote yalitokea kwa Mtume wetu mutukufu Muhammad s.a. w. pekee.

## BISHARA YA SITA.

Katika Isaya 42:1-17 mmeandikwa maelezo kamili juu ya Mtume Muhammad s.a.w. nasi hatuna budi kuyanakili kama ifuatavyo.

1. Tazama mtumishi wangu nimtegemezaye, mteule wangu. ambaye nafsi yangu imependezwa naye, nimetia roho yangu juu yake, naye atawatolea mataifa hukumu.

2. Hatalia wala hatapaaza sauti yake, wala kuifanya isikiwe katika njia kuu.

3. Mwanzi uliopondeka hatauvunja wala utambi utokao moshi hatauzima, atatokeza hukumu kwa kweli.

4. Yeye hatalegea, wala hatakata tamaa, hata atakapoweka hukumu duniani, na visiwa vitaingojea sheri a yake.

5. Mungu Bwana anena, yeye aliyeziumba mbingu na kuzitanda; yeye aliyetandaza nchi na mazao yake; yeye awapaye pumzi watu walio juu yake; yeye awapaye roho wao waendao ndani yake.

6. Mimi. BW ANA. nimekuita katika haki, nami nitakushika mkono na kukulinda na kukutoa uwe agano la watu na nuru ya mataifa.

7. Kuyafunua macho ya vipofu, kuwatoa gerezani waliofungwa.

8. Mimi ni BWANA, ndilo jina langu, na utukufu wangu sitampa mwingine, wala sitawapa sanamu sifa zangu.

9. Tazama mambo ya kwanza yamekuwa nami nayahubiri mambo mapya, kabla hayajatokea nawapasheni habari zake.

10. Mwimbieni BWANA wimbo mpya, na sifa zake tokea mwisho wa dunia, ninyi mshukao baharini, na vyote vilivyomo visiwani, nao wakaao humo.

11. J angwa na miji yake na ipaze sauti zao, vijiji vinavyokaliwa na Kedari; na waimbe wenyeji wa Sela, wapige kelele toka vilele vya milima.

12. Na wamtukuze BWANA, na kutangaza sifa zake visiwani.

13. BWANA atatokea kama shujaa, ataamsha wivu kama mtu wa vita, atalia, naam, atanguruma, atawashinda adui zake.

14. Siku nyingi nimenyamaza kimya, nimetulia. nikajizuia, sasa nitapiga kelele kama mwanamke, aliye katika kuzaa, nitaugua na kutweta pamoja.

15. Nitaharibu milima na Vilima, nitavikausha vyote vimeavyo, nitaifanya mito ya maji kuwa visiwa, na kuyakausha maziwa ya maji.

16. Nitawaleta vipofu kwa njia wasiyoijua, katika mapito wasiyoyajua nitawaongoza, nitafanya giza kuwa nuru mbele yao, na mahali palipopotoka kuwa pamenyoka. Nitawafanyia haya wala sitawaacha.

17. Watarudishwa nyuma, wataaibishwa sana, hao wanaotumainia sanamu za mawe, na kuziambia sanamu za madini, Ninyi ndinyi miungu yetu.

i. Maelezo yale yaliyo katika bishara hii yanamhusu Mtume Muhammad s.a.w. pekee. Aya ya kwanza tu yasema, “Tazama

mtumishi wangu". Bishara hii inalingana sana na Kalima (Tashahud ya Kiislamu) inayosema: Nashuhudia kuwa hapana anayepasa kuabudiwa isipokuwa Mwenyezi Mungu, na nashuhudia ya kuwa Muhammad ni "Mtumishi wake" na "Mtume wake". Wakristo wanasema Yesu alikuwa mwana wa Mungu au Mungu mwenyewe. Hivyo hawezi kuitwa "Mtumishi" wa Mungu. Huyu Mtumishi wa Mungu anayetajwa hapa si mwingine minghairi ya Mtume Muhammad s.a.w.

ii. Kisha bishara inasema "Mteule Wangu" Ingawa maneno haya ya Isaya yalibashiriwa miaka mingi kabla ya kuzaliwa Mtume Muhammad s.a.w. lakini ajabu moja ni hii kwamba jina jingine la Mtume Muhammad s.a.w. ni "Mustafa" ambalo maana yake ni "Mteule".

iii. Bishara inaendelea kusema, "ambaye nafsi yangu imependezwa naye", na katika Kurani tukufu tunasoma, "Hakukuacha Mola wako wala Hakukasirika" (93:4). Maneno haya ya Mwenyezi Mungu yanathibitisha wazi ya kuwa Mtume s.a.w. alipendwa mno na Mola wake.

iv. Ikiendelea mbe!e bishara hii inasema, "Nimetia roho yangu juu yake". Akitimiza ahadi hii Mwenyezi Mungu anasema katika Kurani tukufu. "Na bila shaka hii (Kurani) ni uteremsho wa Mola wa walimwengu. Ameteremka nayo Roho mwaminifu juu ya moyo wako ili uwe miongoni mwa Waonyaji" (26: 193-195). Hii yaonyesha ya kuwa bishara hii yatabiri kuja kwa Mtume Muhammad s.a.w. wala si nabii mwingine.

v. Kadhalika bishara inasema, "Naye atawatolea mataifa hukumu." Ikumbukwe ya kuwa Manabii wote waliokuja kabla ya nabii Muhammad s.a.w. walikuwa manabii wa kitaifa, hivyo walipelekwa kwa mataifa yao pekee. Akitilia mkazo juu ya ujumbe wa kitaifa, Yesu aliwaagiza wanafunzi wake akisema, "Katika njia ya Mataifa msiende, wala katika mji wa Wasamaria msiingie, afadhali shikeni njia kuwaendea kondoo waliopotea wa nyumba

ya Israeli" (Mathayo 10:5). Akizidi kuutetea ujumbe wake wa kitaifa Yesu anasema, "Sikutumwa ila kwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli" (Mathayo 15:24). Hivyo Yesu hawezi kusemwa kuwa alileta hukumu kwa mataifa. Mtume aliyetolea hukumu mataifa ni Muhammad s.a.w. Yeye tu ndiye aliyetumwa kwa mataifa yote duniani. Mwenyezi Mungu anahakikisha ukweli wa jambo hili kwa kusema katika Kurani tukufu: "Hakika Tumekuteremshia Kitabu kwa haki ili upate kuhukumu baina ya watu kama alivyokufahamisha Mwenyezi Mungu" (4.106).

vi. Tukiendelea mbe!e tunaona bishara inasema. "Yeye hatalegea wala hatakata tamaa hata atakapoweka hukumu duniani," Ahadi hii pia Mwenyezi Mungu aliitimiza katika dhati ya Mtume Muhammad s.a.w. pekee. Kwani katika Kurani tukufu Mwenyezi Mungu anasema. "Bila shaka tumekupa ushindi ulio dhahiri", (48.2). Wenye kusoma historia ya dini mbali mbali wanajua ya kuwa miongoni mwa manabii wa Mungu wanaojulikana ni Nabii Muhammad s.a.w. peke yake aliyewashinda maadui zake wote katika uhai wake. Kabla hajafariki dunia, nchi nzima ya Arabia ilikuwa chini ya uongozi wake. Hivyo tunaona mtumishi wa Mwenyezi Mungu anayetabiriwa hapa si mwengine minghairi ya Mtume Muhammad s.a.w.

vii. Maneno ya kifungu cha tano ingawa hatukuandika hapo juu, lakini yanahakikisha kuwa bishara hii imetoka kwa Mungu. Aya ya sita katika bishara hii inasema "Mimi BWANA nimekuita katika haki, nami nitakushika mkono, na kukulinda na kukutoa uwe agano la watu, na nuru ya mataifa" (Isaya 42.6). Ama sehemu hii ni bishara tukufu mno na ambayo muradi wake Mwenyezi Mungu aliutekeleza juu ya Mtume s.a.w. ili kuondoa tashwishi yo yote katika nyoyo za watu. Kuhusu jambo hili Mwenyezi Mungu akamfunulia Mtume wake akisema. "Na Mwenyezi Mungu atakulinda na watu". (5.68).

Na hivyo hasa ndivyo ilivyokuwa, maana kila adui mwasi aliyetaka kumdhuru Mtume s.a.w. Mwenyezi Mungu aliuzuia mkono

wake usimfikie Mtumishi wake wa haki. Mambo hayo hayawezi kusemwa juu ya Yesu. Wakristo wanasema Yesu alishikwa na maadui zake na akauawa juu ya msalaba. Kwa mujibu wa imani hii ya Wakristo inakuwa wazi sana kwamba bishara hii ya Isaya haimhusu Yesu asilani.

viii. Maneno yaliyoandikwa katika aya ya 8 ni haya.
"Wala sitayapa masanamu sifa zangu". Muradi wa maneno haya ni huu ya kuwa ibada ya masanamu haikubaliki na Mwenyezi Mungu na ya kwamba hapo atakapofika huyo Mtumishi wa Mungu sifa za miungu ya uwongo (masanamu) zitatoweka kwa njia iliyo bayana zaidi. Na kusema kweli hivi ndivyo ilivyotokea. Alipodhihiri Nabii Muhammad s.a.w. ibada ya masanamu ilikuwa imesitawi sana hususa katika bara Arabu. Katika nyumba ya Mwenyezi mungu, Al-Kaaba, mliwekwa masanamu yasiyopungua 360. Lakini Muhammad, Mtumishi wa Mungu, aliyachukia masanamu toka utoto wake. Wala hakupata kuyaabudu hata mara moja. Na wakati ulipowadia yeye alifanikiwa katika kuisitawisha dini ya kweli ya Mwenyezi Mungu na akaitakasa tena nyumba ya Mungu kwa kuyavunjilia mbali masanamu yote yaliyokuwemo humo. Na pia kabla hajafariki dunia ibada ya masanamu ilifagiliwa kote Arabuni na watu wote walizama katika kumwabudu Mungu mmoja tu. Ufanisi huu alioupata Muhammad s.a.w. unaonyesha wazi ya kuwa bishara hii ya Isaya inamhusu yeye tu wala si nabii mwinginewe.

ix. "Mwimbieni BWANA wimbo mpya." Hapa ufasaha wa Kurani tukufu umetajwa kama wimbo. Kadhalika waandishi wengi wa Ulaya wakivutiwa na mpango wa maneno ya Kurani tukufu, wameiita Mashairi. Na katika maneno haya ya Biblia, Kurani tukufu imepewa mfano wa mashairi na kwa kuwa ni ufunuo mpya ndio ukaitwa "Wimbo Mpya". Hapa ni lazima ifahamike ya kuwa Yesu hakuleta sheria yo yote mpya. Yeye mwenyewe anasema, "Msidhani ya kuwa nalikuja kuitangua Torati au manabii, la, sikuja kutangua bali kutimiza" (Mathayo 5.:17). Kwa mujibu wa maneno haya ya Biblia, Yesu hawezi kusema alimwimbia BWANA wimbo

mpya, bali alikuja kutimiza sheria ya Musa. Kurani tukufu ndiyo Sheria mpya, na ndio wimbo mpya wa BWANA.

x. Katika maneno haya, “Na waimbe wenyeji wa Sela”, Sela yaashiria kwenye mlima mmoja katika Madina. Neno Sela ni alama nyingine ya kuwa bishara hii inamhusu Mtume Muhammad (s.a.w.) pekee.

xi. Maneno haya, “Ninyi mshukao baharini”, yanaashiria misafara ya wabashiri wa Kiislamu ambao walisafiri katika bahari ili kulieneza Neno la Mungu, Kurani Tukufu, miongoni mwa watu wa visiwa na nchi mbali mbali. Ikumbukwe ya kuwa Waislamu walifanya safari nyingi ili kuweza kuihubiri dini ya Mwenyezi Mungu. Ni kweli ya kwamba Wahubiri wa Kristo pia walisafiri ulimwenguni kueneza dini yao. Lakini ipo tofauti iliyoko baina yao na Wabashiri wa Kiislamu. Waislamu walihubiri ili kutekeleza maagizo ya nabii mtukufu, Muhammad s.a.w. ya kuwa ni wajibu wa kila Mwislamu kuitangaza dini, lakini kwa upande wa Wakristo tunaona ya kwamba ni wao wenyewe walioamua kuhubiri duniani kote bila kuamrishwa na Yesu, bali kwa kufanya hivyo wakaasi amri za Yesu. Katika Mathayo (10;5-6). tunasoma, “Hao Thenashara Yesu aliwatuma, akisema. Katika njia ya Mataifa msiende, wala katika mji wo wote wa Wasamaria msiingie”. Kwa mujibu wa maneno haya, ujumbe wa Yesu haukutumwa kwa ajili ya watu wa mataifa yote.

Hivyo muradi wa msemo huu, “Ninyi mshukao baharini,” haumhusu Yesu wala wanafunzi wake, bali unaashiria safari za Waislamu kwani wao ndio waliopewa amri ya kuyahubiria mataifa yote ulimwenguni. Nasi tunaona visiwa kama vile Indonesia vikiwa mfano mwema miongoni mwa nchi zile zilizoupokea Uislamu kutokana na wabashiri wa Kiislamu waliofika huko toka Arabu.

xii. Maneno ya aya ya 11 yanasema “Jangwa na miji yake na ipaaze sauti zao, vijiji vinavyokaliwa na Kedari, na wakaao katika majabali na waimbe, na wapige kelele kutoka juu ya milima.” Neno hili Kedari lilitotajwa hapa linaashiria ukweli kwamba nabii

anayebashiriwa katika bishara hii atakuwa Mwarabu, maana Kedari ni jina la mmoja wa wana wa Ismaili walioishi katika jimbo la Hijaz, Arabu. Kwa kuwa Yesu hakuwa Mwarabu bishara hii haimhusu. Bishara hii yamhusu Nabii Muhammad s.a.w. kwa sababu yeye ndiye aliyetokana na wazao wa Ismaili walioishi katika Hijaz.

xiii. Katika Isaya 42:13 tunaambiwa ya kuwa nabii anayebashiriwa atapigana vita na maadui zake na ya kuwa yeye atawashinda wote. Historia inashuhudia ya kuwa nabii Muhammad s.a.w. aliwashinda maadui zake wote. Hivyo bishara hii inatimia katika dhati yake.

14. Ama maneno ya aya ya 17 katika mfululizo huu yanatueleza hali ya wenye kuabudu masanamu pindi watakaposhindwa na kuletwa chini ya himaya ya Mungu wa kweli, mwumba wa mbingu na ardhi na vilivyomo baina yao. Bishara hii pia ilitimia sawa sawa katika dhati ya Mtume Muhammad s.a.w. Dini ya Mwenyezi Mungu ilipopata ushindi na maadui wa Waislamu wakaletwa mbele ya Mtume s.a.w., watu hawa walionekana dhalili na walioona haya sana machoni pa wenzi fungwa, kuwatoa wale walioketi gizani katika nyumba ya kufuwao. Yaani masanamu yao hayakuwafanyia cho chote, na mtu yule ambaye hapo mwanzoni walimwita yatima na mnyonge sasa Mwenyezi Mungu akampa ushindi juu yao, nao wamekuwa chini ya mamlaka yake.
Ushindi kama huu hakuupata Yesu, hivyo bishara hii haimhusu.

## BISHARA YA SABA.

Mojawapo ya bishara kubwa inayoashiria kuja kwa Nabii Muhammad s.a.w. ni hii. “Naye atawatwekea bendera mataifa toka mbali, naye atawapigia miunzi tokea mwisho wa nchi. Na tazama watakuja mbio mbio upesi sana. Miongoni mwao hakuna achokaye wala kukwaa; Hakuna asinziaye wala kulala usingizi. Wala mshipi wa viuno vyao hautalegea. Wala ukanda wa viatu vyao hautakatika; Mishale yao ni mikali na pinde zao zote zimepindika. Kwato za

farasi zao zitahesabika kama gumegume. na gurudumu zao kama kisulisuli. Ngurumo yao itakuwa kama ya simba, watanguruma kama wana-simba. Naam, watanguruma na kukamata mateka, na kuyachukua na kwenda zao salama, wala hakuna mtu atakayeokoka. Nao watanguruma juu yao siku hiyo kama ngurumo ya bahari. Na mtu akiitazama nchi, ataona giza na dhiki, nayo nuru imetiwa giza katika mawingu yake" (Isaya 5:26-30).

Maelezo ya bishara hii ni haya ya kwamba wakati utafika ambapo mtu mmoja atainua bendera nje ya Falastina (Palestine). Mtu huyu atayaita mataifa ya ulimwengu nao wataitikia wito wake na kumfuata upesi tena kwa wingi.

Wale watakaomfuata wataacha uvivu na uzembe na watajitoa wakfu kwa imani yao.

Watapigana vita na kwato za farasi zao zitatoa moto kama risasi. Watawashambulia maadui zao kwa kasi, mfano wa kisulisuli au kimbunga. Watawashinda maadui zao kwa njia ambayo hakuna atakayeweza kuwaokoa. Na watafanya haya yote kwa sababu gani? Kwa sababu wataona dunia imejaa giza ambalo lingeondoka tu kwa kila mmoja wao kujitolea kufa na kupona.

Bishara hii nzima inamhusu Mtume Muhammad s.a.w. nayo ilitimia barabara katika dhati yake. Kurani tukufu pia imegusia jambo hili. Nabii Muhammad s.a.w. alidhihiri katika Makka, mbali na Falastina, na akainua bendera yake toka Madina, naye ndiye aliyetoa wito huu kwa ulimwengu wote. "Enyi watu, hakika mimi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu kwenu nyote," (Kurani Tukufu: 7:159). Ni wito wake huu uliowavuta wake kwa waume kote duniani kama nguvu za umeme. Katika uhai wake Yesu hakumbatiza hata mtu mmoja nje ya nyumba ya Waisraeli. Vivyo hivyo. wanafunzi wake wote waliishi hatua chache tu kutoka maskani pa Yesu.

Lakini wafuasi wa Mtume wa Uislamu mwanzoni tu, walitoka sehemu mbali mbali kama vile Yeman, Iran na Uhabeshi. Na miongoni mwa waliosilimu walikuwemo waliokuwa zamani

waabuduo masanamu, Mayahudi na hata Wakristo. Waaminio hao, (Mungu awe radhi nao), kwa kufuatia mwito wa Mtume s.a.w. walijitoa wakfu kwa dini yao na wakadumu katika imani katika kila hali hivi kwamba hata maadui wa dini ya Kiislamu wamelazimika kuusifu uthabiti na ushupavu wa masahaba hao wa Mtume s.a.w. Akitukumbusha jambo hili Mwenyezi Mungu anasema. “Mwenyezi Mungu amewaridhia nao pia wamemridhia,” (9:100). Wafuasi wa Mtume walilazimika kupigana vita kuilinda dini yao, nao humo vitani wakatumia pinde na mishale. Kwato za farasi wao wepesi zilikuwa kama risasi na gurudumu zao kama kinyamkela. Ukali huu wa majeshi ya Waislamu pia umetajwa katika Kurani tukufu. “Naapa kwa (Farasi) wakimbiaji wanaotweta. na kwa wale watoao moto kwa kupiga, tena kwa wale washambuliao wakati wa asubuhi, basi wao wanapeperusha mavumbi, kisha wanaingia ndani ya kundi” (100:2-6). Hizi ndizo sifa za majeshi ya Waislamu na ni ajabu vile zinavyolingana na bishara hiyo ya Isaya tuliyoitaja hapo juu.

## BISHARA YA NANE

Bishara nyingine bayana juu ya kufika kwa Mtume Muhammad s.a.w. imo katika Isaya 62:2. “Nawe utaitwa jina jipya, litakalotajwa na kinywa cha BW ANA”. Ni wazi ya kuwa bishara hii inaashiria kufika kwa dini mpya itakayopewa jina na Mungu mwenyewe katika ufunuo wake.

Madaktari wa Biblia wamekosea sana kwa kudhani ya kuwa bishara hii inahusu kuundwa kwa Kanisa la Kristo. Wanasahau kwamba majina kama “Wakristo” au “ukristo” au majina yale mengine mengi ambayo makundi mbali mbali ya Wakristo wanayatumia, si majina yaliyofunuliwa na Mwenyezi Mungu, bali ni majina waliyojitungia wao wenyewe. Waila bishara hii inasema juu ya jina litakalotoka katika kinywa cha Mungu. Dini ya Kiislamu pekee ndiyo iliyopewa jina “Islamu”, kwa ufunuo wa Mwenyezi Mungu, haya yanathibitishwa na Kurani Tukufu inayosema: “Yeye (Mwenyezi Mungu) aliwaiteni Waislamu tangu zamani na katika (Kurani) hii pia” (22.79). Aya hii ya Kurani Tukufu ina uhusiano dhahiri na bishara hiyo ya Isaya.

Ni kana kwamba Mwenyezi Mungu anasema, “Tulibashiri tangu zamani ya kuwa jina lenu hamtajichagulia ninyi wenyewe bali litatoka Kwetu Sisi. Na leo hii basi tunawaiteni Waislamu.” Jina hili “Islamu” linatokana na neno 'Salm' lililo na maana ya amani. Ikumbukwe ya kuwa katika bishara nyingine Nabii Muhammad s.a.w, ameitwa “Mfalme wa amani” (Isaya 9:6). Ama hii ni bishara ya ajabu mno. Kadhalika juu ya ukweli ya kwamba miongoni mwa dini zote ni Waislamu peke yao wanaotangaza ya kuwa wamepewa jina la “Islamu” na Mwenyezi Mungu ndani ya ufunuo wake - Kurani tukufu. Isaya alitabiri kufika kwa nabii ambaye wafuasi wake watapewa jina na Mwenyezi Mungu kwa njia ya ufunuo. Nabii huyu ndiye Muhammad s.a.w. na Mwenyezi Mungu kawaita wafuasi wake “Waislamu” na dini yake “Islam”.

## BISHARA YA TISA

Injili ya Yohana inatuambia ya kwamba Mayahudi walitazamia ufikaji wa Manabii watatu. Waliwatuma watu kumwuliza Yohana Mbatizaji, “Wewe U nani? Naye alikiri wala hakukana, alikiri kwamba mimi siye Kristo. Wakamwuliza ni nani basi? U Eliya wewe? Akasema, Mimi siye. Wewe u nabii yule? akajibu, La,” (1:19-21).

Kristo, Eliya na Nabii Yule ndio Mitume watatu waliotazamiwa kufika, waliongojewa na Waisraeli. Injili inaeleza ya kwamba Yohana Mbatizaji ndiye Eliya, (Matt.17:10-13, Luka 1: 18), na Kristo ni Yesu. Sasa amebaki mmoja, naye ni Nabii Yule, ambaye si mwingine ila ni Mtume Muhammad s.a.w. maana baada ya Kristo hakuna mtu aliyedai kuwa bishara zake zimo katika Biblia, kisha akafaulu. isipokuwa Mtume Muhammad tu.

## BISHARA YA KUMI

Katika Yohana 14.16 imeandikwa. “Nami nitamwomba Baba naye atawapa Msaidizi Mwingine, ili akae nanyi hata milele”. Tena Yesu alisema, “Hayo ndiyo niliyowambia wakati nilipokuwa nikikaa

kwenu. Lakini huyo Msaidizi, huyo Roho Mtakatifu, ambaye Baba atampeleka kwa jina langu, atawafundisha yote na kuwakumbusha yale niliyowambia". (Yohana 14.25,26). Tena Yesu alisema, "Hata bado nikali ninayo mengi ya kuwaambia, lakini hamwezi kuyastahamili hivi sasa. Lakini yeye atakapokuja, huyo Roho wa kweli, atawaongoza awaite kwenye kweli yote" (Yohana 16:12-13).

Wakristo wanasema "Msaidizi Mwingine" aliyeahidiwa kufika katika Injili ya Yohana si Mtume Muhammad, bali ni Roho Mtakatifu. Waislamu tunajibu hivi:-

(i) Kama Msaidizi huyo ni Roho Mtakatifu, Yesu asingesema, "Yawafaa ninyi mimi niondoke, kwa maana mimi nisipoondoka, huyo Msaidizi hatakuja kwenu," (Yohana 16:7).
Yesu asingesema hivyo kwa sababu huyo Roho Mtakatifu wa Wakristo alikuweko duniani siku zote hata kabla ya Yesu kuzaliwa. Yesu alipobatizwa, Roho huyo alimshukia (Math. 3:16).
Tena kabla ya kuwaacha wanafunzi wake aliwapulizia, akawaambia, "Pokeeni Roho Mtakatifu" (Yohana 20:22). Ilmuradi wanafunzi wa Yesu walikuwa na Roho huyo kabla ya kufa kwa Yesu, au tuseme, kabla hajatengana nao.

(ii) Zile alama zilizobainishwa na Yesu hazipatikani katika Roho Mtakatifu, kama (a) kuwaongoza watu kwenye kweli yote na kuwakumbusha maneno ya Yesu, (b) kumtukuza Yesu (Yohana 16:14).

Mtume Muhammad s.a.w. ndiye aliyekuja miaka mingi baada ya Yesu akileta sheria yenye amri nyingi za Sheria za zamani, na mengi yaliyo mapya, ili kukamilisha Sheria. Kurani yenyewe inadai kuwa ni Sheria iliyo kamili (sura 5:4.) Tena Mtume s.a.w. alimtukuza Yesu na kumkinga na masingizio yote ya Mayahudi na Wakristo, akamwonyesha kama mtu mwema asiye na dhambi, na pia kuwa hakufa kifo cha laana msalabani.

Ikiwa Wakristo wangali wanaongozwa na Roho Mtakatifu, mbona basi wanayo makanisa mengi yanayopingana? Je kila

kanisa lina Roho Mtakatifu wake? Kisha Roho Mtakatifu wa kila kanisa anakuwa adui wa Roho Mtakatifu wa kanisa jingine? Hata watu wa kanisa moja hawachelei kuwaita Wakristo wa kanisa jingine “Wapinzani wa Kristo na watu wa Shetani.” Au je, Yesu akitoka mbinguni atakwenda kwa nani na atamuacha nani katika wale ambao wamekwisha pata ubatizo au wanaopewa misa na sakramenti nyingine mara kwa mara, lakini wanaitwa na Wakristo wa kanisa jingine “Wapinzani wa Kristo na watu wa Shetani”? Hakika ni hii ya kuwa hawana dalili yo yote ya kuhakikisha kuwa yule Roho wa kweli aliyeahidiwa ni Roho Mtakatifu wanayedhani kuwa wanaye anawaongoza. Ni jambo wasiloweza kuhakikisha; yaliyobaki ni madai ya mdomo tu.

## BISHARA YA KUMI NA MOJA.

Katika barua aliyoandika Yuda (Yuda 1: 14-15) tunasoma maneno haya, “Na Henoko, mtu wa saba baada ya Adamu, alitoa maneno ya unabii juu ya hao akisema, angalia, Bwana alikuja na Watakatifu wake, maelfu maelfu, ili afanye hukumu juu ya watu wote, na kuwaadhibisha wote wasiomcha Mungu, kwa ajili ya kazi zao zote za upotevu walizotenda bila kumcha Mungu, na kwa ajili ya maneno magumu yote ambayo hao wenye dhambi wasiomcha Mungu wameyanena juu yake”.

Maneno ya juu yamenakiliwa toka katika tafsiri mpya ya Biblia ya Kiswahili iitwayo “Union Version”. Katika tafsiri hii mpya wameandika "Bwana alikuja na watakatifu wake maelfu maelfu" Lakini katika tafsiri za zamani katika Kiswahili, mpaka mwaka 1949 walitafsiri “Elfu kumi za watakatifu wake”. Kila mtu atafahamu ya kwamba hayo si tofauti ya maneno tu, bali maana na mradi pia vimegeuzwa. Maana bishara hiyo inabashiri kufika kwa Mtume Muhammad s.a.w. pamoja na watakatifu elfu kumi, na ilitimia wakati Mtume alipoingia Makka na idadi hiyo ya watakatifu. Hakuna Nabii ye yote aliyetimiliwa na bishara hiyo isipokuwa Muhammad s.a.w. Ni kwa sababu hiyo mapadre wamependa kubadili maneno hayo

ili kuwadanganya na kuwavuruga wasomao Kiswahili. Juu ya hayo Injili za Kiingereza bado zina maneno “Ten Thousand of his saints” (Elfu kumi za watakatifu wake).

## BISHARA YA KUMI NA MBILI.

Bishara hii yenye nguvu imo katika Mathayo 21:33-40. Hii ni mojawapo ya methali za Yesu ambamo ndani yake mna utabiri wa kufika Mtume Mtukufu. Bishara yenyewe ni hii:-
“Kulikuwa na mtu mwenye nyumba naye alipanda shamba la mizabibu, akalizungushia ua, akachimba shimo la shinikizo ndani yake, akajenga mnara akapangisha wakulima akasafiri. Wakati wa matunda ulipokuwa karibu akawatuma watumishi wake kwa wale wakulima, wapokee matunda yake. Wale wakulima wakawakamata watumishi wake, huyu wakampiga na huyu wakamwua, na huyu wakampiga kwa mawe. Akawatuma tena watumishi wengi kuliko wa kwanza, ikawa tena vile vile. Mwisho akamtuma mwanawe kwao, akisema watamsitahi mwanangu.

“Lakini wale wakulima walipomwona yule mwana, wakasemezana wao kwa wao, Huyu ni mrithi haya na tumwue, tuutwae urithi wake, Wakamkamata wakamtupa nje ya shamba la mizabibu, wakamwua. Basi atakapokuja yule bwana wa shamba la mizabibu atawatendaje wale wakulima? Wakamwambia, Atawaangamiza vibaya wale wabaya, na shamba la mizabibu atawapangisha wakulima wengine, watakaomlipa matunda kwa wakati wake. Yesu akawaambia, Hamkupata kusoma katika maandiko, Jiwe walilolikataa waashi, hilo limekuwa jiwe kuu la pembeni. Kwa sababu hiyo nawambia, Ufalme wa Mungu utaondolewa kwenu, nao watapewa taifa lingine lenye kuzaa matunda yake. naye aangukaye juu ya jiwe hilo atavunjika , na yeyote ambaye litamwangukia litamsaga tikitiki. Wakuu wa makuhani na Mafarisayo waliposikia mifano yake, walitambua ya kuwa anawanenea wao. Nao walipotafuta kumkamata, waliwaogopa makutano, kwa maana wao walimwona kuwa nabii.”

Katika methali hii iliyo nzuri Yesu ameeleza historia ya mfululizo wa kuja kwa Mitume. Ni wazi hapa kwamba shamba la mizabibu ndiyo ulimwengu, wakulima maana yake ni walimwengu kwa jumla, matukio ambayo bwana wa shamba alitaka kuvuna ndiyo wema, uaminifu na ucha-Mungu, watumishi ndiyo manabii wa Mungu waliokuja duniani mmoja baada ya mwingine; mwana ndiye Yesu aliyekuja baada ya mfululizo wa manabii wengi. Mwana huyu aliadhibiwa na wakulima. Baada ya kusema mambo haya, Yesu ameendelea kunena juu ya "Jiwe" walilolikataa waashi, hilo limekuwa "jiwe kuu la pembeni." Jiwe lililokataliwa ndiyo wazao wa Ismaili, waliodharauliwa na wana wa Isihaka. Kulingana na bishara hii ya Yesu, mtu mmoja angekuwa jiwe kuu la pembeni - "Muhuri wa Manabii," katika lugha mashuhuri ya Qur'an tukufu - hangekuwa nabii wa cheo cha chini, bali m'bora wa manabii atakayeleta Sheria ya mwisho na kamili toka kwa Mwenyezi Mungu. Kuinuliwa kwa Nabii toka katika nyumba ya Ismaili lilionekana jambo geni, kwani wengi katika mfululizo wa manabii wa hapo mbele walitoka katika nyumba ya Isihaka (Israel). Lakini Yesu anasisitiza ya kuwa Mwenyezi Mungu ataondoa ufalme wake kutoka nyumba ya Israeli na kuwapa wana wa Ismaili, watakaotoa matunda yake; yaani wana wa Ismaili ndiyo watakaokuwa taifa litakalodumisha ucha-Mungu na ibada ya Mwenyezi Mungu duniani. Kila mtu anaweza kuona hapa ya kuwa hapana mtu yeyote aliyedai utume baada ya Yesu, na akafanikiwa, isipokuwa Mtume mtukufu Muhammad s.a.w. Ni yeye ambaye mafundisho yake yalihitilafiana na dini ya Mayahudi na akavunja kabisa nguvu za dini hiyo. Ni yeye ambaye taifa lake lilidharauliwa na kuchukiwa. Kama tulivyosema hapo mbele, nabii Muhammad s.a.w. ndiye mjumbe wa Mungu wa pekee aliyejaaliwa kushinda maadui zake wote katika uhai wake, hivyo ni yeye tu ambaye ndiye lile jiwe ambalo yeyote aliyeanguka juu yake alivunjika-vunjika na yeyote liliyemwangukia likamsaga tikitiki. Wakristo wamekosea sana kwa kudhani Yesu ndiye "Jiwe" linalotajwa hapa. Lakini wanasahau ya kuwa Yesu alikuwa Mwisraeli, hali yeye amesema "Ufalme wa

Mungu utaondolewa kutoka kwa Waisraeli na kupewa taifa jingine," yaani Waismaili. Isitoshe, ikiwa jiwe ni Yesu, basi ingefaa kufahamishwa aliwasaga akina nani tikitiki?

## BISHARA YA KUMI NA TATU.

Katika Mathayo 23:38-39 tunasoma "Angalieni nyumba yenu imeachwa hali ya ukiwa. K wa maana nawaambieni, Hamtaniona kamwe tangu sasa, hata mtakaposema, Amebarikiwa ajaye kwa jina la Bwana."

Aya hii inaashiria ya kuwa Yesu ataachana na watu wake nao hawatamwona tena mpaka wao watakaposema "Amebarikiwa ajaye kwa jina la Bwana".

Kadhalika, hapa pamebashiriwa majilio mawili. Moja baada ya kifo cha Yesu, na hili lingekuwa kama Mungu mwenyewe kuja duniani. Jingine ni kuja kwa Yesu mara ya pili. Kama inavyobainishwa na bishara yenyewe, yule ajaye kwa jina la Bwana atafika kabla ya kurudi kwa Yesu mara ya pili. Tumekwisha eleza ya kuwa yule ajaye kwa jina la Bwana anafanana na Musa. Hivyo bishara hii ya Yesu ikiambatana na ukweli wa kuja kwa Mtume Muhammad s.a.w. na dini ya Kiislamu, inathibitisha ya kuwa katika mpango wa Mwenyezi Mungu. Yesu hakuwa nabii wa mwisho na wala kuja kwake hakukusudiwa kumfikisha mwanadamu kwenye kiwango cha mwisho cha maendeleo ya kiroho. Kazi hii angeifanya "Yule ajaye kwa jina la Bwana," ambaye ndiye angekuwa msingi wa maendeleo makubwa ya kiroho. Ingekuwa upotevu dhahiri kufikiri ati baada ya kuja "Yule ajaye kwa jina la Bwana" Yesu angerudi tena ili apate sifa ya kuwa nabii aliye chanzo cha maendeleo ya upeo katika dini ya Mwenyezi Mungu. Yesu mwenyewe analiweka jambo hili wazi mbele ya macho yetu anaposema. "Hamtaniona kamwe tangu sasa mpaka mtakaposema, Amebarikiwa ajaye kwa jina la Bwana" (Mathayo 23:39).

Ikumbukwe pia ya kuwa Yesu hakuwa nabii mleta Sheria, bali alikuwa masihi wa nabii Musa na alikuja kutilia nguvu Sheria ya Musa. Hivyo katika bishara hii Yesu anawatangazia watu wake akisema. “Wala hamtamwona nabii na Masihi kama mimi mpaka atakapokuja nabii mfano wa Musa kwanza, nanyi muwe wenye kumkubali.” Hivi ni kama kusema hapana Masihi ila kwanza aje nabii mleta sheria mpya. Kadhalika maneno haya yatathibitisha ya kuwa mpango wa Mwenyezi Mungu wa kuleta manabii duniani katika muda uliowekwa si jambo lenye kikomo. Ama ndugu Wakristo wanaipotosha sana bishara hii ya Yesu ya kuendelea kwa unabii, kwani wao husema hapana nabii baada ya Yesu.

Tukirudia sehemu ya pili ya bishara yenyewe, yaani kuja kwa Yesu mara ya pili, tunaona ya kuwa ni wale tu ambao kwanza watamkubali Nabii mfano wa Musa atakayetangulia kurudi kwa Yesu, ndio watakaomwona na kumtambua Yesu arudipo duniani. Asiyemkubali yule nabii aliye mfano wa Musa, hataweza kutambua kurudi kwa Yesu. Kwa nini? Kwa sababu Yesu arudipo duniani atakuwa miongoni mwa wafuasi wa yule nabii mfano wa Musa. Hivyo ni wazi kuwa watu miongoni mwa wale watakaokuwa wamemwamini yule nabii mfano wa Musa, wataweza kukubali na kutambua kuja kwa Yesu mara ya pili. Yesu ajapo mara ya pili hatakuwa nabii mwenye kujitegemea, bali atakuwa mfuasi mwaminifu na kielelezo kilicho bayana cha yule nabii mfano wa Musa. Na daraja la mwisho la wokovu wa mwanadamu halina chanzo chake ila ni pale alipofika yule nabii mfano wa Musa - na Yesu ajapo atakuwa masihi wa nabii huyo naye ataitilia nguvu Sheria yake.

Baada va kutoa maelezo juu ya majilio mawili vanayoashiriwa katika bishara hii ya Yesu. sasa panabaki swali moja kujibiwa ili kutimiza muradi wa bishara yenyewe. Swali lenyewe ndilo hili. Je, ni mtu gani aliyedai unabii na akafaulu baada ya kifo cha Yesu? Ni ukweli unaokubaliwa na kila mwenye kujua ya kuwa hapana mtu hata mmoja aliyedai kuwa nabii wa Mungu kwa walimwengu na akapata ufanisi, baada ya Yesu, ila Muhammad s.a.w. Mtume

Mtukufu wa Uislamu. Nabii Muhammad s.a.w. ndiye aliyekuwa mfano kamili wa nabii Musa. Miongoni mwa ishara tukufu zinazotubainishia ukweli wa jambo hili, ni ile Sheria mpya, Kurani tukufu, aliyopewa Mtume Muhammad s.a.w. ili kuwa mwongozo kwa watu wote. Katika sifa hii manabii wawili, Muhammad na Musa (amani na baraka za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao), wanafanana. Nabii Musa alipewa Sheria ya Mungu -Torati, ambayo kwa kuitimiza Yesu alikuja. (Mathavo 5:17); lakini baadaye akabashiri kufutika kwa Sheria hiyo kwa kusema: “Kwa sababu hiyo nawaambia Ufalme wa Mungu utaondolewa kwenu, nao watapewa taifa jingine lenye kuzaa matunda yake” (Mathayo 21:43). Kwa hivyo, maneno haya ya Yesu aliyowaambia wana wa Israeli, hayapingi ukweli huu kwamba nabii Musa na nabii Muhammad wamefanana sana.

Naam, na Muhammad s.a.w. ndiye nabii yule aliyetabiriwa na Yesu kuja kwa jina la Bwana. Nabii Muhammad s.a.w. alifunuliwa kila jambo kwa jina la Mwenyezi Mungu. Sura zote za Kurani tukufu zaanza kwa jina la Mwenyezi Mungu. Isitoshe yeye mwenyewe Mtume Muhammad s.a.w. alianza kila jambo kwa jina la Mwenyezi Mungu. Na kama kila mwanadamu afuate mfano huu mtukufu - kama itakavyokuwa katika siku za ushindi wa dini ya Kiislamu - basi hapo dunia nzima itajaa fahari ya jina la Bwana. Ndipo Yesu akawataka watu wake waseme, “amebarikiwa ajaye kwa jina la Bwana,” na kumkubali Mtume wa Uislamu. Ni wale tu miongoni mwa watu wa Yesu, watakaofuata maagizo haya na kusilimu, ambao watapewa nuru katika macho yao ya kiroho nao wataweza kumwona na kumtambua Yesu arudipo.

Ni lazima ikumbukwe ya kuwa kuja kwa Yesu mara ya pili baada ya kufika yule nabii Mfano wa Musa. siyo maana yake ya kuwa ni Yesu yule yule wa Nazareti, ambaye atashuka kutoka mbinguni kama wadhanivyo Wakristo. La, hasha. Muradi sahihi wa kurudi kwa Yesu, au masihi, mara ya pili ni kwamba kutakuja nabii mfano wa Yesu kuja kutilia nguvu sheria ya nabii Yule, mfano wa Musa, kama vile Yesu mwenyewe alivyokuja kutilia nguvu sheria

ya Musa. Yaani, kama vile nabii Musa na Muhammad s.a.w. wanavyofanana kwa kuleta Sheria. vivyo hivyo Yesu na masihi wa nabii Muhammad wanafanana kwa kutoleta sheria - bali kutilia nguvu sheria iliyopo. Kama tulivyosema hapo mbele, kule kurudi kwa Yesu mara ya pili kunakotajwa katika bishara hii kunathibitisha ya kuwa mlango wa utume haukufungwa na hivyo manabii wa Mungu wataendelea kuletwa duniani pakiwa na haja. Na Yule mjumbe aliyetabiriwa kuja baada ya nabii aliye Mfano wa Musa, angekuja kufanya kazi kama ya Yesu na angekuwa mfano wa Yesu.

Wale wanaosema ati ni Yesu yule yule wa Nazareti atakayeshuka toka mawinguni, wanakosea sana. Yesu alikufa fofofo. Kufuatia sheria za Mwenyezi Mungu za maumbile, wafu hawarudi tena duniani. Ni sheria hizi ambazo zimepiga marufuku kwamba mtoto azaliwe na kisha kurudi tena tumboni mwa mamaake. Hivyo ile ndoto ya kuwa Yesu wa Nazareti atarudi tena duniani na kuwa Masihi wa Nabii Muhammad s.a.w. haitatimia kamwe. Isitoshe, wazo hili la kipagani, lina maana ya kwamba Mwenyezi Mungu (Mungu apishe mbali) hawezi kuumba tena, kwani kashindwa kuumba nabii mwingine mfano wa Yesu hata ikamlazimu kumfufua Yesu, mwana wa Mariamu, na kumleta tena duniani awe masihi wa nabii Muhammad s.a. w. Bila shaka wazo hili lenye makosa litakataliwa na kila mwenye akili. Mtu anaweza kuuliza, na mambo yakiwa hivi basi Yesu atarudi duniani kwa njia gani?

Kurudi au kudhihiri kwa Yesu mara ya pili, kungetokea kwa njia ya kawaida tu. Yeye angezaliwa kama vile walivyozaliwa manabii wengine wa Mwenyezi Mungu. Pia kuna alama nyingi, kama tutakavyoona baadaye, zilizotabiriwa ili kutujulisha wakati hasa atakapofika, na pia kutuwezesha kumtambua. Jambo lenye maana sana ni kukumbuka ya kuwa Yesu ajapo tena hatakuwa nabii mwenye kujitegemea, bali atakuwa mfuasi mwaminifu na kielelezo safi cha yule nabii Muhammad s.a.w.

## KUJA KWA NABII MUHAMMAD S.A.W.

Kwa fadhili za Mwenyezi Mungu bishara zote tulizozieleza katika kitabu hiki zilitimia barabara kwa kuja kwake nabii Muhammad s.a.w. Biblia na Kurani tukufu vyote vinasema nabii Muhammad ni wa damu ya Nabii Ibrahim a.s. Biblia yasema nabii Ibrahim alikuwa na wake Watatu-Sarah. Hajira na Katura. Hajira alimzaa Ismaili na Sarah akamzaa Isihaka. (Mwanzo. 16:10-12 na 17:19). Isihaka aliishi nchi ya Kanani na ndiye baba wa Mayahudi. Kufuatia ahadi ya Mwenyezi Mungu kwa Ibrahim manabii wengi na hata wafalme walizaliwa katika nyumba au kizazi cha Isihaka, kama vile Musa, Haruni, Joshua, Isaya, Daudi, Suleimani na Yesu (Mungu awe radhi nao). Ismaili aliishi katika nyika za Parani, yaani Arabu. Kufuatia ahadi ya Mwenyezi Mungu kwa Ibrahim, Ismaili alikuwa baba wa watoto 12 wanaume. Siku za utoto wa Ismaili, nabii Ibrahim aliamriwa na Mwenyezi Mungu kumchukua mwanawe pamoja na mkewe Hajira na kuwaacha katika bonde tambarare la Makka. Ibrahim akafanya hivyo, naye akamchukua mwanawe hali yu mdogo na kumwacha na mama yake pamoja na chakula kidogo katika bonde tambarare karibu na Kaaba.

Kwa mara kadha Bi Hajira alimwuliza nabii Ibrahim kwa nini anafanya hivyo? Safari ya mwisho nabii Ibrahim akaitikia kuwa anafanya hivyo kwa amri ya Mungu. Hajira akasema kama ni hivyo, basi, Mwenyezi Mungu hawezi kutuangamiza. Nabii Ibrahim aliondoka pale na akiwa mbali kidogo na mkewe na mwanawe alielekea Kaaba na kuinua mikono yake juu akaomba dua hii, “Mola wetu, hakika mimi nimewakalisha baadhi ya wazao wangu katika bonde lisilozaa karibu na Nyumba yako tukufu, Mola wetu, ili wasimamishe sala. Basi Ujaalie mioyo ya watu ielekee kwao na Uwaruzuku matunda ili wapate kushukuru” (Kurani Tukufu 14:38).

Baada ya nabii Ibrahim kuondoka, na chakula na maji kuwaishia Bi Hajira na mwanawe Ismaili walisikia sana kiu. Hapo Hajira akahangaika sana kutafuta maji. Katika kufanya hivyo

alipanda na kushuka vilima viwili mara kadha. Vilima hivi ndivyo Safaa na Marwa. Baadaye alijitupa kwa Mwenyezi Mungu na akaomba sana. Maombi yake yalikubaliwa na Mwenyezi Mungu akabububujisha chemchem ardhini karibu na mahali alipokuwa Ismaili. Maji hayo yalibububujika kwa mlio wa "Zam, Zam, Zam". Mpaka hivi leo kisima hiki kitakatifu kinaitwa Zam-Zam.

Baadaye Mwenyezi Mungu alimwamuru nabii Ibrahim kujenga tena Kaaba, ambayo ndiyo nyumba ya kwanza kujengwa kwa ajili ya ibada ya Mungu mmoja. Kazi hii aliifanya pamoja na mwanawe Ismaili ambaye sasa alikuwa mtu mzima. Walipokuwa wakijenga, nabii Ibrahim na Ismaili waliomba dua hii kwa Mungu:

"Ee Mola wetu, Utupokelee, hakika Wewe Ndiwe Mwenye kusikia, Mwenye kujua. Ee Mola wetu, Utufanye tuwe tujitupao Kwako, na miongoni mwa wazao wetu pia Uwafanye watu wajitupao Kwako, Na Utuonyeshe njia za ibada yetu na Utuelekee, bila shaka Wewe ndiwe Mwelekevu, Mrehemevu.

Ee Mola wetu, mwinue Mtume kati yao atokaye miongoni mwao, awasomee Aya Zako, na kuwafundisha Kitabu na hekima, na kuwatakasa. Hakika Wewe ndiwe Mwenye nguvu, Mwenye Hekima." (Kurani Tukufu, 2':128-130).

Miongoni mwa watu waliovutiwa na Kaaba na kuhamia Makka ni kabila la Jurhum. Mtemi wao mkuu aliitwa Madhadh mwana wa Amr. Ismaili na mamaake Hajira (Mungu awe radhi nao) ndio waliokuwa wakaazi wa kwanza wa Makka. Ismaili alimwoa binti wa Mtemi huyu na akazaa naye wana 12. Majina yao ndiyo haya. Nebayothi, Kedari, Abduli, Milesamu, Mishma, Duma, Masa, Hadadi, Tema, Yeturi, Nafishi na Kadema (Mwanzo. 25:13-16). Hawa ndio waliokuwa wakuu wa makabila ya Waarabu waliotawanyika katika Bara Arabu au Paran. Waarabu wengi hudai kuwa wa ukoo wa Kedari mwana wa Ismaili. Tangu hapo zamani Waarabu waliiheshimu sana Kaaba na mila ya Ibrahim nayo waliilinda sana. Baada ya kufariki Ismaili ulinzi wa Kaaba ukawa

mikononi mwa Nafishi (Nabit). Alipofariki Nafishi Kaaba ikawa inalindwa na babuye Madhadh, na hivyo kwa muda mrefu kabila lake Jurhum likawa ndilo lenye kutawala sehemu hiyo ya nchi takatifu. Utawala huu baadaye ulirudi mikononi mwa wazao halisi wa Ismaili kwa njia ya shujaa mmoja aitwaye Qusaiyy. Yeye alikuwa mtu mwenye maarifa sana na aliweza kuwakusanya watu wengi wa ukoo wa Ismaili chini ya serikali moja. Akaupa heshima zaidi mji wa Makka na kulinda kwa uangalifu sana nyumba ya Mungu yaani Kaaba. Ujasiri na maarifa yake yaliwafanya watu wake wampe jina la Kuraishi yaani mkusanyaji. Hilo ndilo jina la kabila miongoni mwao alimozaliwa Mtume Muhammad s.a.w. kama alivyoomba nabii Ibrahim a.s.

Ni wazi kutokana na maelezo haya kuwa nabii Muhammad s.a.w. ni wa damu ya baba wa manabii, Ibrahim. Naye alikuja ulimwenguni baada ya Wana wa Israeli kumsahau Mwenyezi Mungu na kuyatupilia mbali mafundisho ya Musa. Kadhalika walivunja maagano ya nabii Ibrahim na Mwenyezi Mungu ya kwamba kila mtoto wa kiume ni lazima afanyiwe tohara. Hivyo ufalme wa Mwenyezi Mungu ukaondolewa kwao na ukapewa taifa jingine.

Taifa hili ni taifa la wana wa Ismaili ambao waliyaheshimu maagano tuliyoyataja na wakawatahiri wanaume wao. Hii ni alama ya kimwili kuonyesha utii kwa Mwenyezi Mungu kama alivyofanya nabii Ibrahim. Na katika utii wa kiroho tunaona ya kuwa nabii Ibrahim na mwanawe Ismaili, baba wa Waarabu, waliomba Mungu ainue mtume miongoni mwa wazao wao atakayewafundisha Kitabu. hekima na kuwatakasa. Kama matokeo ya dua hii, Mwenyezi Mungu alimwinua nabii Muhammad s.a.w. kutoka miongoni mwa wazao wa Ismaili. Akampa kitabu (Kurani Tkufu) hekima na ucha - Mungu ili kuwaletea walimwengu utii wa kiroho, hekima, na utakaso ambao ndiyo matunda hasa ya ufalme wa Mungu ulioondolewa kutoka kwa wana wa Israeli. Mtume s.a.w. mwenyewe amesema, “Mimi ndiyo dua ya Ibrahim” (Jarir na Asakir).

Nabii Muhammad s.a.w. alizaliwa tarehe 20 April, 571 A.D. Kabila lake lilikuwa Kuraishi na ukoo wake Banu Hashim. Akiwa mtoto yatima alianza maisha yake kwa unyonge. Katika ujana wake alikuwa mwaminifu hata akaitwa "AL-Amin". Ingawa ibada ya masanamu ilistawi sana wakati huo, yeye hakupata kuyaabudu hata mara moja na aliyachukia sana. Alipopata umri wa miaka 40 alipewa cheo cha utume. Na kama walivyotabiri Yesu na manabii wengine wa zamani, akapewa Sheria mpya (Kurani Tukufu).

Yeye pamoja na wafuasi wake waaminifu walitaabishwa sana na maadui zao hata baadaye wakalazimika kuhamia Madina. Huko walistawi sana. Wakapigana vita na maadui wachokozi na kwa fadhili za Mwenyezi Mungu maadui hao waliangamia wote. Baadaye akiwa na wataktifu wake 10,000 nabii Muhammad s.a.w. aliushika mji wa Makka bila ya kumwaga damu. Maadui zake wote wakaletwa mbele yake hali ni wenye kukata tamaa. Yeye aliwasamehe wote.

Kabla ya kuaga dunia alikuwa amepata ufanisi mkubwa ajabu. Wala hapana nabii mwingine aliyefanikiwa hivyo akiwa hai. Na alipofariki bara zima la Arabu lilikuwa limeingia katika dini ya Mwenyezi Mungu ya Uislamu, yaani "Kujitupa kwa Mwenyezi Mungu" kama alivyoomba nabii Ibrahim a.s.

Naam, huyu ndiye Muhammad mtume na nabii wa Mungu aliyepewa Sheria na pia akahama mji wake kuepa uovu wa maadui na baadaye akafaulu sana na akafa hali yu Mfalme na mpendwa wa Walimwengu. Katika haya yote alifanana sana na nabii Musa - la, bali yeye alikuwa mfano halisi wa nabii Musa.

Wale ndugu zetu wanaodhani kuwa nabii anayetabiriwa katika bishara ya Mathayo 23:39 ni nabii mwingine wala si nabii Muhammad s.a.w., basi watuambie ni nabii yupi aliyetabiriwa kuja kwa jina la Bwana baada ya Yesu?

## SEHEMU YA PILI

# HADHRAT AHMAD A.S. MASIHI WA MTUME MUHAMMAD S.A.W.

Madhumuni ya makala hii haitatimia kama nisitaje hapa, kwa ufupi, kuja kwa Masihi, mfano wa Yesu, katika umati wa Mtume Mtukufu Muhammad s.a.w., ambaye ameahidiwa na Mtume mwenyewe. Ikumbukwe hapa ya kuwa Mtume Muhammad s.a.w. amefananishwa na Musa ndani ya Kurani Tukufu. Kama nabii Musa alileta sheria mpya na Mtume Muhammad s.a.w. pia alileta sheria mpya. Mwenyezi Mungu anasema :-
"Hakika Sisi Tumewatumieni Mtume aliye shahidi juu yenu kama Tulivyompeleka Mtume kwa Firauni" (Kurani Tukufu 73:16).

Aya hii inatuambia wazi wazi ya kwamba Mtume Muhammad s.a.w. anafanana na nabii Musa. Kwa hiyo imelazimishwa ya kwamba kama alivyodhihiri Masihi mmoja katika umati wa Musa ndivyo hivyo atakavyotokea Masihi mwingjne katika umati wa Mtume Muhammad s.a.w. vile vile; na kwa ajili hii Mtume Muhammad s.a.w. alisema ya kwamba:-

"Wawezaje kuangamia umati ambao mwanzoni mwake nipo mimi na mwishoni mwake atadhihiri Masihi". (Ibni Maja).

Kurani Tukufu vile vile inaashiria juu ya kufika kwa Masihi mmoja katika umati wa Mtume Muhammad s.a. w. Katika aya hii:-

"Na anapotajwa mwana wa Mariamu kwa namna ya mfano (Yaani mfano wake atafika) ndipo watu wako wanaupigia kelele" (Kurani Tukufu 43:58).

Sasa ni wazi ya kwamba wafuasi wa Mtume Mtukufu Muhammad s.a.w. waliahidiwa kuja kwa Masihi, mfano wa mwana

wa Mariamu. Agano jipya la Biblia vile vile linatuambia ya kwamba Masihi mwana wa Mariamu atarudi duniani mara nyingine (Mathayo 24:4-41).

Sasa juu ya kuja Masihi mfano wa Yesu tunaona kuwa bishara hii ya Biblia, Kurani Tukufu na hadithi ya Mtume Muhammad s.a.w. ilitimia kwa ufikaji wa Hadhrat Ahmad a.s. wa Qadian. Kama tulivyoona, kuja kwa Masihi wa nabii Muhammad s.a.w. kumefananishwa na kurudi kwa Yesu mara ya pili. Kazi ya Masihi huyu ingekuwa kuimarisha na kutilia nguvu Sheria ya yule nabii mfano wa Musa. Tumeona kuwa nabii huyu si mwingine ila nabii Muhammad s.a.w. Na masihi wake si mwingine ila Hadhrat Ahmad.

Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. alizaliwa katika kijiji cha Qadian, India, mnamo Febuari 13, 1835. (14 Shawwal, 1250.) Babu zake walitokea Uajemi. Tangu utotoni Hadhrat Ahmad a.s. alionyesha alama za utukufu na alitumia wakati wake mwingi katika kumkumbuka Mwenyezi Mungu na kusoma Kurani Tukufu na vitabu vingine vya dini. Alichukizwa sana kuona Uislamu unavyotukanwa na maadui zake, hususa Wakristo na wafuasi wa dini ya Kibaniyani (Arya Samaj). Waislamu walikuwa katika hali ya nyuma na kutojali dini yao hivi kwamba walishindwa kuyapinga mashambulio maovu ya maadui wa Uislamu.

Hadhrat Ahmad a.s. kwanza aliandika makala magazetini kuutetea Uislamu. Baadaye aliona nabii Muhammad s.a.w. katika ndoto. Jambo hili lilimtia moyo na akaandika kitabu maarufu sana kiitwacho Baraahine Ahmadiyya. Katika kitabu hiki Hadhrat Ahmad a.s. alitoa hoja madhubuti kurudisha mashambulio ya maadui wa Uislamu hata mtu yeyote hakuthubutu kuzijibu hoja zake.

Katika mwaka wa 1890 Mwenyezi Mungu alimfunulia kwamba yeye ndiye Masihi aliyeahidiwa na pia Mahdi. Wakristo, Wa-Arya Samaj na mashekhe wa Kiislamu wote wakaungana

pamoia kumpinga Seyidna Ahmad a.s. alipotangaza jambo hili. Alifanya mijadala mingi iuu ya mas'ala ya dini na akawabwaga wapinzani wake wote vibaya sana kwa hoja zake zenye nguvu juu ya ubora wa dini ya Kiislamu. Watu waliompinga wakazidisha uovu wao hata wakamfikisha kortini kwa mashtaka ya uwongo ya kuua. Huu ulikuwa mwaka wa 1894 ambapo ile ishara mashuhuri ilivyotabiriwa zamani ilitimia kuthibitisha kufika kwa Masihi aliyeahidiwa. Ishara hii ilikuwa kupatwa kwa jua na mwezi katika mwezi wa Ramadhan. Hadhrat Ahmad akajulishwa kabla na Mwenyezi Mungu kuwa atashinda kesi yake. Hivyo ndivyo ilivyotokea na Colonel Douglas aliyeisikiliza kesi hiyo hakumpata Seyidna Ahmad a.s. na kosa lolote Jaji huyu mwenye haki alipewa jina Pilato.

Jumuiya ya Ahmadiyya ikazidi kupata nguvu. Mwaka wa 1908 kikapigwa chapa kitabu chake mashuhuri kiitwacho "Yesu katika India" (Jesus in India). Katika kitabu hiki alithibitisha kwa ushahidi kwamba Yesu aliepuka kifo cha laana cha msalaba na akasafiri hadi Kashmir, India. Huko akawahubiria wana wa Israeli walioishi kule na baadaye akafa na akazikwa huko mtaa wa Khanyar, Srinagar. Kashmir. Kwa kufuatia ufunuo wa Mwenyezi Mungu. Hadhrat Ahmad aliligundua kaburi la Yesu.

Hadhrat Ahmad a.s. alibashiri maafa ya tauni. matetemeko na vita vitano vikuu vya dunia. Maafa haya yote yalitokea kama alivvobashiri. Matetemeko ya dunia bado yanaendelea kadhalika vita viwili vimekwisha tokea na vingine vimebakia.

Mwaka 1903 pakatokea nabii wa uwongo aliyeitwa Dr. J. A. Dowie wa Amerika. Mtu huyu alijidai kuwa yu Eliya aliyerudi mara ya pili duniani. Seyidna Ahmad a.s. alimwandikia barua na humo akamwomba Mwenyezi Mungu amwangamize yule aliye mwongo na mzushi baina ya watu wawili hao na amwache hai yule mkweli (wakati huo Hadhrat Ahmad alikuwa miaka 15 zaidi na akiwa na

afya si nzuri kuliko Dr. Dowie). Mzushi huyu wa Amerika alirudisha majibu ya ujeuri na matusi na tangu hapo utajiri wake na wafuasi wake wakaanza kupungua. Alikufa mwaka wa 1907 akiwa maskini asiye na rafiki wala wafuasi. Mji wake wa Zion aliouanzisha ulififia na mauti yalimvamia hali yu mwenda wazimu aliyepooza.

Hadhrat Ahmad aliendelea na mahubiri kwa nguvu sana na wafuasi wake wakazidi kuongezeka. Katika mwaka wa 1904 alitangaza kwamba Krishna, Buddha na wengineo walikuwa ni mitume wakweli wa Mwenyezi Mungu, kwani kila taifa lilipelekewa mjumbe ila tu, mafunzo ya wajumbe hao kama vile ya Yesu yalichafuliwa na watu wa baadaye. Mwaka wa 1905, kulitokea tetemeko kubwa la dunia lililoleta vifo vingi katika sehemu kadha za India. Tetemeko hili lilipotukia Hadhrat Ahmad alikuwa akiandika maneno haya ya ufunuo wake “Mwonyaji mmoja alifika duniani, lakini dunia haikumpokea, lakini Mwenyezi Mungu atampokea na atadhihirisha ukweli wake kwa mashambulio makali.” Miongoni mwa bishara zake maelfu kuna utabiri juu ya mabalaa na maafa mengi ulimwenguni tangu mwaka wa 1914 ambayo mwisho wake ataangamizwa yule “Dajjal” aliyetajwa na nabii Muhammad (s.a.w.) – na huu ni utawala wa kinyama, kufuru, uasherati na madhambi – kisha mwishowe Uislamu utashinda na kutawala milele. Akiongea juu ya vita vya tatu vya dunia Hadhrat Ahmad alitabiri kuwa vitakuwa vikali hivi kwamba vitakaribia kuangamiza uhai wote ulimwenguni lakini Uingereza hata kama itapata hasara kubwa, itakuwa miongoni mwa washindi. (Haqiqat-ul-Wahi).

Mnamo mwaka huo huo Hadhrat Ahmad alijulishwa na Mwenyezi Mungu kuwa umri wake umekaribia kwisha. Hata hivyo hakupuuza kazi zake tukufu za kuitetea dini ya Kiislamu na kubomoa misingi ya dini za uwongo. Alianza kuandika kitabu chake cha 80 kiitwacho “Paeghame Sulha” – yaani Ujumbe wa Amani, lakini tarehe 20 mwezi Mei 1908 Mungu alimkumbusha tena kwamba mwisho wake wakaribia.

Yapata saa nne u nusu asubuhi tarehe 26 Mei, mwaka wa 1908 alitamka maneno haya mara mbili "Mpenzi Mola Wangu" na akafariki mwenye umri wa miaka 74. Na huyu ndiye aliyekuwa Ahmad Masihi aliyeahidiwa kuja siku za mwisho kama mfano wa Isa mwana wa Mariamu.

Jambo la kustaajabisha ni ule mlingano uliopo katika nyakati walizofika wajumbe hawa watukufu wa Mwenyezi Mungu, Musa, Yesu, Muhammad na Ahmad (amani na baraka za Mungu ziwe kwao wote). Tukichukua silsila ya nabii Musa tunaona yeye mwenyewe alizaliwa yapata 1275 B.C. Na masihi wake Yesu, akazaliwa yapata miaka 1269 baada ya hapo. Na tuchunguapo silsila ya nabii Muhammad s.a.w. tunakuta ya kwamba alizaliwa 570 AD., na Masihi wake aliyeahidiwa, Hadhrat Ahmad, akazaliwa 1835 AD., miaka 1265 baadaye. Hivyo tukilinganisha silsila hizi mbili tunaona pana muda sawa unaomtenganisha Yesu kutoka kwa Musa na Ahmad kutoka kwa nabii Muhammad s.a. w. Hii yatosha kwa wenye akili kutambua jinsi bishara tulizotaja zilivyotimia sawa sawa.

Hapana shaka ya kuwa mtu anayemkataa nabii Muhammad anamkataa Yesu na Biblia yote kwa jumla, kwani bishara zote tulizozichunguza tumeona zimetufikisha kwenye ukweli usioepukika wa nabii Muhammad s.a.w. Sasa ni juu ya wenye akili kutafakari juu ya jambo hili na kutupilia mbali karaha zao zisizo na msingi ili kuifuatia njia iliyonyoka - "Islamu".

## BISHARA ZA KUJA KWA MAHDI ALIYEAHIDIWA

Hapa chini tunanakili baadhi ya bishara nyingi alizotabiri nabii Muhammad s.a. w. juu ya kufika kwa Masihi na Mahdi.
Tunatumai ya kuwa bishara hizi zitaondolea mbali shaka yo yote katika nyoyo za watafutao haki.

1. Hakika Mwenyezi Mungu atamwinua kwa ajili ya umati huu mwanzoni mwa kila karne yule Atakayehuisha upya Dini na kuitilia nguvu" (Abu-Daud, Ja1ada 2, uk. 241). Hadhrat Ahmad a.s. ndiye mtu wa -pekee kudai kuwa Mujaddid wa kame ya kumi na nne.

2. Masihi aliyeahidiwa ataitwa "Nabiyyullah" (Nabii wa Mungu) (Muslim, Jalada 2, uk. 515).

3. Huyo Mahdi na Masihi atakuwa yule yule mtu mmoja (Ibni Majah, Jalada 2, uk. 257).

4. Kuja kwa Yesu mara ya pili kutakuwa katika njia ya Imam kutokana na Waislamu wenyewe (Bukhari, Jalada 2, uk 490).

5. Huyo Masihi ataua nguruwe na kuvunja msalaba. (Bukhari, Jalada. 2. uk. 159). Bishara hii inaonyesha ya kuwa Masihi atawaokoa Waislamu toka katika upotevu na kudhihirisha ubovu wa imani ya Kikristo.

6. Huyu Mahdi atafutilia mbali vita vya kidini (Musnad Ahmad Ibni Hanbal, Jalada 2, uk. 411).

7. Katika wakati wa Mahdi elimu itatapakaa na kuzidi mno, na watu watachanganyana zaidi. (Tirmidhi).

8. Katika wakati huo, kutabuniwa njia mpya za usafirishaji na ngamia watakuwa wenye kuachwa (Mishkat-ul-Masabih).

9. Imani itapungua na hapatabaki cho chote katika Uislamu ila jina tu nayo Kurani tukufu itabakia maandiko matupu (Mishkat-ul-Masabih. uk. 38. Kanz-ul-Ummal. Jalada. 6. uk. 43).

10. Waislamu watakaposikia kufika kwa Mahdi basi yawapasa wafanye haraka kuungana naye hata kama katika kufanya hivyo itawalazimu kutambaa juu ya barafu ili kufika aliko yeye. (Kanz-ul-Ummal, pia maelezo ya Ibni Hanbal, Musnad, Jalada. 6. uk. 29. 30).

11. Mataifa ya Kikristo yatakuwa yenye nguvu nyingi ulimwenguni. (Hujajul Karama. Tirmidhi na vinginevyo).

12. Wakati huo mwezi na jua vitapatwa katika mwezi ule ule wa Ramadhani (Dar-Qutni. Sunan, Jalada. 8. uk. 188). Jambo hili lilitukia mnamo tarehe 13 na 28 mwezi wa Ramadhani mwaka 1894.

13. Atakuwa na masahaba 313 (Ghayat-ul-Maqsud). Hivi ndivyo ilivyokuwa, na majina ya hao masahaba 313 yamehifadhiwa.

14. Atakuwa mmoja wa mapacha (Ibni Arabi. Sharah Fusus-ul-Hikam). Hadhrat Ahmad a.s. alizaliwa pacha lakini dadake akafariki baada ya kuzaliwa.

15. Atawakumbusha watu mafundisho ya Yesu (Kurani Tukufu. 61:7).

16. Wakati huo kutatokea tauni (Ikmal-ud-Din. uk. 348). Tauni iliambukia mwaka 1902 A.D.

17. Masihi atadhihiri upande wa mashariki (Ibni Majah).

18. Atadhihiri katika mahali paitwapo Kadaa (Jawahir- ul-asrar. uk. 56). Wenyeji wa zamani wa Kadian hupaita Kadaa.

19. Atatokana na ukoo wa Kiajemi (Bukhari. Bab-ul-fitan).

20. Wakati huo kutakuwa na Manabii wa uwongo (Bukhari, Bab-ul-Fitan, Muslim Bab-ul Fitan).

21. Uislamu utakuwa na karne tatu za utukufu, kisha utapaa mbinguni kwa miaka elfu moja (Bukhari. Jalada, 4 juu ya Kurani tukufu 86:2). Ndiyo kusema ustawi wa pili wa Uislamu utaanza mwanzoni mwa karne ya kumi na nne ya Hijrah. (Ahmad - The Promised Messiah and Mahdi. uk. 13, 14).

Hapo juu tumetaja baadhi ya hadithi za Mtume Muhammad s.a. w. juu ya kufika kwa Masihi na Mahdi aliyeahidiwa. Masihi na Mahdi huyu atakuwa mfuasi wa Nabii Muhammad s.a.w. naye atakuwa ni mfano wa Yesu - hata ataitwa Isa bin Mariamu. Akitaja juu ya jambo hili Mtume s.a.w. alisema “Mtakuwaje atakaposhuka mwana wa Mariamu kati yenu naye ndiye Kiongozi wenu atakayetokana nanyi! (Bukhari).

Hivyo kuja kwa Yesu mara ya pili si jambo lililo na shaka hata kidogo. Bali lilitimia katika umati wa “yule ajaye kwa jina la Bwana” yaani Muhammad s.a.w.; na umati huu ni wenye kudumu milele. Hata Mtume s.a.w. akasema: “Umati ulio na mimi upande mmoja na Masihi mwana wa Mariamu upande wa pili hauwezi kuangamia”. (Ibni Majah).
Mwishoni mimi nawaomba watu wote kutafakari kwa bidii juu ya madhumuni ya kitabu hili; hususa juu ya sehemu yake ya pili. Mwenyezi Mungu Afumbue macho ya wote wanaoupenda haki, amin.

***AMANI NA BARAKA ZA ALLAH VIWE JUU YA MTUME MUHAMMAD S.A.W.***